Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Pili - Tarehe 31 Oktoba, 2012

(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 15

Ahadi ya Kupandisha Kituo cha Afya Mwandoya Kuwa Hospitali

MHE. HENRY D. SHEKIFU (K.n.y. MHE. LUHAGA J. MPINA) aliuliza:-

Je, utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ya kupandisha hadhi ya kituo cha afya Mwandoya kuwa Hospitali aliyoitoa wakati wa kampeni za uchaguzi mwaka 2010 imefikia hatua gani kwa sasa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, alitoa ahadi ya kupandisha kituo cha Afya Mwandoya kuwa na hadhi ya Hospitali kwa kukiwezesha kutoa huduma za upasuaji. Lengo kubwa la uamuzi huu ni kusogeza huduma ya afya ya msingi kwa wananchi wote kwa ubora unaokubalika na kwa gharama nafuu. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto walio chini ya umri miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2011 Serikali imepeleka jumla ya shilingi 71,029, 183 kwa ajili ya kuboresha miundombinu mbalimbali ya kituo hicho. Kazi ambazo zimefanyika hadi sasa ni kupeleka umeme wa gridi ya Taifa hadi kwenye kituo, ujenzi wa jengo la upasuaji lenye kitanda cha kufanyia operesheni, ujenzi wa wodi ya watoto yenye uwezo wa kuchukua vitanda 14, ununuzi wa Kitanda kimoja cha watoto njiti *(premature babies),* ununuzi wa gari la kubebea wagonjwa (*ambulance*) pamoja na kupeleka watumishi kwenye mafunzo mbalimbali katika vyuo hapa nchini ili kuwajengea uwezo wa kutoa huduma bora.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 241.3 kwa ajili ya kununua vifaa tiba na dawa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kikiwemo kituo cha afya cha Mwandoya.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kama inavyoeleweka katika mpango wa MMAM ni kwamba kila Kata inapaswa kuwa na kituo cha afya na kila kijiji kuwa na zahanati. Kwa mpango huu ambao Waziri ameusema ziko hospitali na vituo vya afya vingi ambavyo vinahitaji kufunguliwa kikiwepo hiki cha kwenye jimbo la Mheshimiwa Luhaga Mpina.

Sasa Serikali inachukua hatua gani kutoa ratiba kamili za kuhakikisha kwamba vituo vya afya pamoja na zahanati zinafunguliwa na wananchi wanajua ni kipindi gani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naonba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Shekifu kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba sera ya Serikali imeagiza na inasimamia utekelezaji wa ujenzi wa zahanati katika kila kijiji na uwepo wa kituo cha afya katika kila kata ili kusogeza huduma hizi kwa wananchi kwenye maeneo haya, na pindi zinapofunguliwa tunahakikisha kwamba raslimali watu kwa maana ya waganga na wauguzi inakuwepo ili tuweze

kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo kufunguliwa kwa kituo ni pindi tu kazi hizo zinapokamilika na uwepo wa vifaa tiba.

Kwa hiyo, kituo cha afya cha Mwandoya ambacho tayari sasa kimeishakamilika na mwaka huu wa fedha kimeishatenga zaidi ya shilingi milioni 241.3 pindi raslimali watu na vifaa tiba vikikamilika taratibu zote zitakuwa ziko sawa tayari kwa kuanza huduma kwenye maeneo yale ambayo yamekusudiwa.

SPIKA: Ahsante, tunaendelea. Hawa hawakusimama mwanzoni! Haya Dkt. Hamisi Kigwangala.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa vituo vya Afya katika mpango wa MMAM pamoja na Zahanati zake vimekuwa vikijengwa kwa wingi sana katika nchi yetu, na kwa kuwa vituo hivi vimekuwa *under staffed* lakini pia na kwa kuwa Serikali imeongeza jitihada ya kusomesha wataalam katika sekta ya afya na haiwaajiri, napenda kujua nini kauli ya Serikili kuhusiana na ukweli kwamba wanahitimu madaktari zaidi ya 1,000 lakini wanaajiriwa chini ya 100.

Ni lini madaktari hawa wataajiriwa ili kwenda kujaza raslimali watu katika vituo vinavyojengwa katika mpango huu wa MMAM?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Hussein Alli Mwinyi, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Serikali imeongeza idadi ya Wanafunzi wanaoingia katika vyuo vya afya. Mwaka uliopita walihitimu wanafunzi 7,000 na vibali vya ajira vilivyopatikana mwaka huo huo vilikuwa ni 9,000 lakini tulishindwa kuwapata wataalam hao kwa sababu kubwa ya wengi wao kutokuwa tayari kwenda kufanyakazi katika maeneo ya pembezoni mwa nchi. Kwa hiyo, tunachoweza kusema ni kwamba Serikali itaendeleza jitihada za kudahili wanafunzi wengi zaidi katika vyuo vyetu na lengo ni kufikia wanafunzi 10,000 kwa mwaka. Vilevile Serikali itaendelea kutoa vibali vya ajira, lakini kwa kuwa tatizo kubwa ni kuwa-*retain* wafanyakazi hawa katika maeneo ambayo ni magumu, Serikali ina mpango wa kuleta hiyo inayoitwa posho ya mazingira magumu *(hardship allowance)*ili hatimaye tuweze kuwabakiza hawa wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba taratibu hizo zinaendelea ili hatimaye tuondokane na tatizo hili ambalo limeikabili nchi yetu. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya.

Na. 16

Matatizo Yaliyoko Kwenye Sekta ya Elimu Nchini

MHE. MHONGA S. RUHWANYA aliuliza:-

Sekta ya Elimu imekumbwa na matatizo mengi sana ikiwemo wanafunzi kujifunza wakiwa wamekaa chini:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza mahitaji halisi ya madawati katika shule zote nchini?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kila mwanafunzi anajifunza katika mazingira mazuri ikiwemo kupata vitabu pamoja na walimu bora?

(c) Je, ni nini upungufu na mahitaji halisi ya vifaa kama madawati, vitabu na mahitaji ya walimu katika mkoa wa Kigoma?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naonba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Septemba mwaka 2012 takwimu zetu zinaonesha kuwa mahitaji halisi ya madawati katika shule za Msingi nchini ni 3,339,985, yaliyopo ni 2,029, 310 na upungufu tulionao ni 1,310, 675. Kwa upande wa shule za Sekondari mahitaji halisi ya madawati ni 1,648, 858, yaliyopo ni 1, 231,440 na upungufu tulionao ni 417,418.

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anajifunza katika mazingira mazuri ikiwemo kupata vitabu pamoja na Walimu bora. Katika kutekeleza azma hii kupitia Mpango wa Elimu ya Sekondari MES na

Mpango wa Elimu ya Msingi MEM, Serikali imekuwa ikipeleka fedha za ruzuku ya uendeshaji (*Capitation Grant*) kwa shule zote za Serikali nchini. Asilimia 50 ya fedha hii ni kwa ajili ya ununuzi wa vitabu kwa shule za Sekondari na asilimia 40 ni kwa ajili ya ununuzi wa vitabu kwa shule za Msingi.

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali ilipeleka katika Halmashauri zote nchini jumla ya shilingi 52,618,736,118 kwa ajili ya uendeshaji *(Capitation)* zikiwemo shilingi 19,410,768,698 kwa shule za Msingi na shilingi bilioni 33,207,967,420 kwa shule za Sekondari.

Kwa mwaka 2012/2013 jumla ya shilingi bilioni 93 zimetengwa kwa ajili ya *Capitation* zikiwemo shilingi bilioni 52 (52,545,074,000) kwa shule za Msingi na shilingi bilioni 41 (41,076,941,000) kwa shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, suala la upatikanaji wa Walimu wenye sifa stahiki limepewa kipaumbele cha kutosha na Serikali ambapo kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 Walimu wanaoajiriwa ni wale tu wenye sifa zitakazokidhi kupewa mafunzo ya ualimu, wamepata mafunzo katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na wamefaulu mafunzo yanayotolewa vyuoni.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kigoma kwa mwaka wa 2012 mahitaji halisi ya madawati kwa shule za Msingi ni 141,108, yaliyopo sasa ni 89,206 na upungufu uliopo ni 51,902. Kwa upande wa shule za Sekondari mahitaji ya madawati ni 90,599, yaliyopo ni 51,905 na upungufu ni 38,694. Aidha, mahitaji ya Walimu kwa shule za Msingi ni 8,448, waliopo ni 6,522 na upungufu ni 1,930. Kwa upande wa shule za Sekondari mahitaji ya Walimu ni 2,097, waliopo ni 1,065 na upungufu ni 1,032.

Mheshimiwa Spika, hali ya vitabu vya kiada kwa upande wa shule za Msingi viko katika uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi wanne (1:4) na kwa upande wa shule za Sekondari vimefikia uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi saba (1:7).

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo hayo niliyoyataja ya ukosefu wa Walimu, vitabu, maabara na madawati, njaa pia humfanya mtoto ashindwe kuwa makini katika kusikiliza masomo yake. Ni nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba watoto wanapatiwa angalau uji shuleni?

(ii) Matatizo niliyoanisha yanapatikana zaidi katika shule zetu za Serikali na si katika shule binafsi, hivyo tunaona kabisa tofauti kubwa ya uelewa na ufaulu wa wanafunzi.

Je, Serikali kwa kutotatua matatizo haya haraka haioni kuwa inachangia kushuka kwa elimu nchini, mdondoko wa wanafunzi *(drop out),* utoro, watoto kumaliza shule bila kujua kusoma na kuandika, lakini vilevile Serikali inachangia nchi yetu kuwa na matabaka ya utoaji wa elimu kwa watoto? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu langu la msingi juu ya upatikanaji wa madawati, vitabu na uwepo wa Walimu katika shule za msingi na Sekondari nchini. Lakini pia unataka kujua ni lini Serikali itatoa angalau uji katika shule zetu.

Suala la chakula kwenye shule zetu za Msingi na Sekondari za Kata, tumeendelea kuhamasisha wananchi kwenye maeneo yao kuona namna ambavyo vijana hawa au watoto wetu wanapata chakula shuleni na kwa kufanya hilo inaweza kuleta mafanikio makubwa sana kwa kuwa mtoto atapata muda mzuri wa kusoma akiwa amepata lishe, na pale ambapo inawezekana Serikali kupitia vyanzo vya Wizara kwa maana ya TAMISEMI tukipeleka katika Halmashauri inaweza kuwa *top up* ya fedha ambayo wao wametenga kwenye Mabaraza yao ili kusaidia kupeleka vyakula shuleni.

Eneo ambalo tunatoa chakula ni kwa shule za bweni ambazo ziko rasmi na zimetambuliwa na tuna orodha yake na kwa sasa tume-*improve* vizuri tu kuhakikisha kwamba shule zote za bweni zinapata chakula vizuri na katika eneo hilo hatuna matatizo makubwa.

Eneo la pili ambalo pia Mheshimiwa Mbunge anataka kuona namna ambavyo tunaweza tukaondoa matatizo tuliyo nayo na kusema kwamba kwa kufanya hivyo Serikali inaweza kuwa inasababisha matabaka mashuleni. Kwanza nataka nikatae kwamba Serikali haina lengo la kuweka matabaka mashuleni katika utoaji elimu, lengo letu ni kila mtoto wa Kitanzania apate elimu ya kutosha iliyo sawa na

mtoto mwingine bila kujali matabaka hayo ambayo yanaweza kuwa yamejitokeza katika maeneo husika.

Tunachokifanya ni kuhakikisha kwamba tunaratibu vizuri shule zetu za Msingi na za Sekondari kuona kwamba matatizo yote yaliyopo yanaratibiwa kwenye ngazi ile ile ambapo pia tuna maafisa elimu wa wilaya kwenye kila Halmashauri na Afisa Elimu wa Mkoa hatimaye sisi TAMISEMI tukiyapata tunaweza kwenda kuyafanyia namna ambavyo tunaweza kuhakikisha kwamba maeneo haya hayapati matatizo makubwa na wala hakutakuwa na matabaka yoyote yale. *(Makofi)*

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Serikali ina mashamba ya misitu ya mbao na vilevile Serikali ina mfuko wa uwezeshaji na kuna vijana kila wilaya hawana kazi na wana ujuzi wa kutengeneza madawati. Kwa nini Serikali isitumie mfuko wa uwezeshaji ikawakopesha vitendea kazi na ikawapa magogo ndani ya mwezi mmoja tu wakatengeneza madawati kila wilaya ikawa na madawati kwenye kila shule na watoto wakayakalia? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Magogo ni ya kwako? *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Mchemba, Mbunge wa Iramba kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Serikali inayo misitu na misitu ile bado inaendelea kuhifadhiwa lakini tumeigawa mingine inamilikiwa na Serikali za vijiji, mingine inamilikiwa na Serikali za wilaya, lakini iko misitu ya Hifadhi za Kitaifa. Misitu hii imetolewa utaratibu wa namna ya kupata mbao kwa shughuli mbalimbal ikiwewo na jamii yenyewe iweze kunufaika pia. Kwa hiyo, kama Halmashauri itapata utaratibu wa namna ya kupata mbao hizo kwa ajili ya kutengeneza madawati jambo hilo linawezekana. Sisi TAMISEMI tunapokuwa na fedha tuliyoitenga kwa ajili ya madawati hatununui madawati *centrally,* tunapeleka katika Halmashauri zake. Kwa hiyo, Halmashauri zenyewe zina mipango yao na kufuata utaratibu wa uvunaji ambapo Mwenyekiti wa Kamati ya Uvunaji katika kila Halmashauri ni Mkuu wa Wilaya. Jambo hili linaweza kutelekezwa katika *level* ile bila matatizo yoyote yale. *(Makofi)*

Na. 17

Utaratibu wa Kuwasimamisha Watumishi Wanaopatikana na Kesi

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI (K.n.y. MHE. SELEMAN BUNDARA) aliuliza:-

Utaratibu wa kuwasimamisha kazi watumishi wa umma wanaopatikana na hatia za ubadhirifu, wizi, ufujaji wa mali za umma na matumizi mabaya ya madaraka ili kutoa fursa wapelelezi wafanye kazi yao kwa haki na uhuru na kuzuia watuhumiwa hao kuharibu ushahidi umeondolewa:-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizofanya utaratibu huo kuondolewa?

(b) Je, Serikali inasema nini kwa watumishi walioshtakiwa kwa tuhuma za aina hiyo ambao kesi zao hazijaisha lakini bado wanaendelea na kazi kwenye ofisi zao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu la Mheshimiwa Seleman Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwasimamisha kazi watumishi wa umma wanaokabiliwa na tuhuma za ubadhirifu, wizi, ufujaji wa mali za umma na matumizi mabaya wa madaraka haujaondolewa. Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298, Kanuni za Utumishi za mwaka 2003 na Kanuni Bora za Utendaji katika Masuala ya Nidhamu za mwaka 2007 zinaeleza kwa kina utaratibu wa hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa mtumishi wa umma anayetuhumiwa kutenda kosa la kinidhamu au la jinai. Kwa hiyo, utaratibu huo haujaondolewa.

Taratibu hizi zinaonesha aina ya makosa na namna yanavyopaswa kushughulikiwa. Aidha, uamuzi wa kumsimamisha mtumishi kazi unafanyika kwa kuzingatia uzito wa tuhuma au kosa husika na athari za kosa hilo kwa mtumishi husika na jamii kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na ufafanunuzi wa Kanuni nilizozitaja kwenye kipengele (a) cha swali hili, kusimamishwa kazi kwa mtumishi wa umma kunategemea kosa alilolifanya na mazingira ya kazi. Endapo uwepo wake kazini kwa mtumishi anayetuhumiwa kutaathiri uchunguzi wa kesi atapaswa kusimamishwa kazi kupisha uchunguzi, na kama uwepo wake kazini hautaathiri uchunguzi mtumishi huyo hatasimamishwa kazi. Pia ikumbukwe kwamba mwajiri yeyote hapaswi kuendelea na hatua zozote za kinidhamu kwa mtumishi anayetuhumiwa wakati kesi yake ipo mahakamani.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, imekuwa kawaida sasa kwa Serikali kwa watumishi ambao wanafanya ubadhirifu katika halmashauri moja kuwatoa na kuwapeleka kwenye Halmashauri zingine.

Je, Serikali haioni kwamba tabia hii inawafanya hawa watumishi waendeleze vitendo vya ubadhirifu katika Halmashauri nyingine ambazo wanapelekwa?

Swali la pili, kwa kuwa kesi nyingi sana zinazowahusu hawa Watumishi zinachukua muda mrefu kumalizika na wao wakiwa wanaendelea kufanya kazi katika vituo vyao au katika vituo vingine vya kazi.

Je, Serikali inafanya nini kuhakikisha kwamba kesi hizi zinaisha kwa haraka ili sasa watumishi hawa wasiendelee kufanya ubadhirifu kama ambavyo sasa imekuwa ni kawaida yao? *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimwia Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mchuchuli kama ifuatavyo:-

Kuhusu kuhamisha watumishi ambao wanatuhumiwa kwa tuhuma mbalimbali. Kwanza, inatakiwa Halmashauri husika wanapomwona mtumishi yeyote anatuhuma ya aina fulani au amefikishwa mahakamani ni bora wakaiarifu Wizara husika. Kwa mfano watumishi wa halmashauri ni vyema wakaiarifu TAMISEMI. Wasipoiarifu TAMISEMI inafanya uhamisho wakati wowote, kwa hiyo hawatakuwa na habari kwamba mtumishi huyo amefanya au hajafanya ubadhirifu. Kwa hiyo, ni vyema Halmashauri zikatoa taarifa mapema kabla mtumishi huyo hajahamishwa.

Pale inapogundulika kwamba mtumishi fulani amehamishwa wakati anatuhuma katika sehemu fulani Wizara husika au TAMISEMI mara nyingi huwa wanamrudisha kule akajibu tuhuma zake kwanza halafu ndipo aende kwenye kituo kingine kipya. Kwa hiyo, ni vyema Halmashauri zikahakikisha kwamba zinatoa taarifa hizo mapema.

Kuhusu kesi kuchelewa hili ni suala la mahakama, kwa hiyo, si busara kuingilia mahakama kwamba kesi hizi mzifanye haraka na msizifanye haraka. Hivyo ni vyombo viwili tofauti. Kwa hiyo, ni vyema tukaziachia mahakama zikatimiza wajibu wake mpaka kesi hizo zitakapoisha ndipo watuhumiwa wanaweza kuhamishwa au kupelekwa sehemu yoyote au kuadhibiwa kulingana na makosa yao.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa watumishi wanaosimamishwa baada ya kuonekana wana matatizo haki zao wanazostahili kupata na zingine ambazo zinasimamishwa huwa huwa zinaainishwa. Kwa kuwa haki hizo zimekuwa zikipishana kati ya watumishi na watumishi wanaposimamishwa kazi.

Je, Serikali iko tayari sasa kupeleka waraka kwa waajiri ili haki hizo ambazo zinatolewa zifahamike kwa watumishi wote wanapopatikana na matatizo ya namna hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo kama ifuatavyo:-

Kuhusu haki za watumishi wanaosimamishwa kazi, sheria zipo na hapa naomba tu niwaeleweshe Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna kusimamishwa kazi na kuna kupumzishwa kazi. Kwa hiyo, sheria zipo tofauti. Mtumishi akisimamishwa kazi ana haki ya kupata nusu ya mshahara wake, lakini anapopumzishwa kazi ni *discretion* ya mwajiri kwamba amlipe kiasi gani. Anapumzishwa kazi *(suspension)* ili kupisha uchunguzi.

Kwa hiyo, pale ni *discretion* ya mwajiri. Lakini sheria zinatamka wazi kabisa kama nilivyosema kwamba ziko sheria za utumishi, Kanuni za Utumishi, zote hizi zinajieleza wazi kabisa, tatizo ni utekelezaji tu wa wale ambao wanahusika. Kwa hiyo, niziase tu Halmashauri na mamlaka za nidhamu kuhakikisha kwamba wanasoma vizuri zile sheria za kazi ili kusiwe na utofauti wowote katika maamuzi.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa, sheria ya sasa ambayo inampa mshitakiwa aliyekuwa mtumishi mshahara mzima na kesi inachukua muda mrefu tofauti na sheria ya zamani ambayo mshitakiwa anasimamishwa na kupewa nusu mshahara na mashauri yanachukua muda mrefu. Je, Serikali haijaona ili kuokoa Halmashauri nyingi hasara za kulipa watu ambao hawafanyi kazi kurejesha sheria ya zamani ya kupewa nusu mshahara? *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ufafanuzi wa suala la watumishi kupewa mishahara nusu au mshahara mzima.

Katika Kanuni za utumishi, vifungu vya 36, 37 na 38 vinajieleza wazi kwamba mtumishi ambaye anasimamishwa kazi analipwa nusu mshahara, mtumishi ambaye anakuwa *suspended, interdiction* na *suspension* ni vitu viwili tofauti.

Kwa hiyo, kwanza tutofautishe hivyo, yule ambaye anasimamishwa kazi analipwa nusu mshahara kama kawaida, yule ambaye anawekwa pembeni kwa ajili ya kupisha uchunguzi anaweza akalipwa mshahara kamili kwa sababu pale hujampa *interdiction.*

Kwa hiyo, sheria hizi ziko wazi kabisa, ila tutambue kwamba kuna mwingine anapisha tu uchunguzi na mwingine anasimamishwa kwa ajili ya kosa fulani. Sheria hizi mbili zipo na zinajieleza kwa hiyo ni vyema tu waajiri wakazisoma hizo sheria na wakatoa maamuzi ambayo ni *uniform* kwa sehemu zote.

Na. 18

Usimamizi wa TASAF Zanzibar

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS aliuliza:-

Mradi wa *TASAF* unasimamiwa kwa ushirikiano wa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Je, kwa upande wa Zanzibar mradi wa *TASAF* unasimamiwa na Wizara gani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mradi wa *TASAF* unasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mkurugenzi wa Uratibu katika ofisi hiyo ndiye anayehusika na uratibu wa shughuli zote za *TASAF* chini ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar.

TASAF imeingia mkataba wa makubaliano na Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na kwa kujidhihirisha kuwa utekelezaji wake unazingatia malengo ya mradi. Vilevile tuna Kamati ya Uongozi Unguja na Pemba ambazo zinapitisha maombi ya miradi yote ya wananchi katika maeneo hayo.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wa Tanzania Bara kawaida miradi hii huwawakilisha wananchi wake kupitia Halmashauri zao. Je, Wabunge wa Zanzibar huwawakilisha wananchi wao kupitia eneo gani katika miradi hii ya *TASAF? (Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Serikali za Mitaa Tanzania Bara unawashirikisha Wabunge katika vikao ambavyo ndivyo Halmashauri ndiyo inayoamua. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inao utaratibu wa Serikali za Mitaa

ambayo ndiyo inayofanya kazi tofauti kidogo na ule utaratibu wa Bara.

Kwa hiyo, nawashauri Waheshimiwa Wabunge kutoka Zanzibar wawasiliane na Kamati inayohusika kule Unguja na Pemba pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kujua jinsi wanavyoweza kushiriki na kutoa mawazo yao kuhusu masuala hayo. *(Makofi)*

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa *interest* kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Mheshimiwa Waziri hawezi akasaidia Kamati hii kwenda kukaa na *TASAF* Zanzibar ili kuondoa hayo matatizo ambayo yanaonekana ni sugu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, sidhani kama hili jambo la *TASAF* linahusiana sana na marekebisho ya Katiba ama sivyo Katiba itakuwa kitabu kikubwa kweli.

Ninachofikiri ni kwamba zile Kamati zilizopo sasa Kamati ya Pemba na ya Unguja inashirikisha Wawakilishi ambao ndio wanashughulika na maendeleo ya maeneo yao kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar. Sioni tatizo kuzungumza na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili Wabunge waweze kushirikishwa kwa sababu ni katika maeneo hayo tutapata maendeleo. Lakini sidhani kama jambo hili linahitaji Katiba.

SPIKA: Nilivyoelewa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tulichoelewa ni kwamba hapa kwetu tuna Kamati ya Katiba, Utawala na Sheria. Kwa hiyo alikuwa anasema hiyo

iende kule ikakutane na *TASAF* na Kamati ya kule. Ndivyo alivyosema. Sivyo, hivyo Mheshimiwa Kombo.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Ndiyo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunieleweshe. Ile Kamati ya Sheria na Katiba ya hapa ina haki ya kwenda kutazama miradi ya *TASAF* Zanzibar. Kwa sababu fedha za *TASAF* hapa zinasimamiwa na hiyo Kamati ya Bunge.

Kwa hiyo, Kamati ya Bunge ikitaka kwenda Zanzibar kuangalia miradi ile ni sawa sawa kabisa haina matatizo yoyote. (*Makofi)*

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa madhumuni ya Kanuni ya 39(1) na 39(9) na kwa mujibu wa jibu la Waziri wa Nchi

SPIKA: Kanuni gani?

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Kanuni ya 39(1)

SPIKA: Ya kanuni zetu?

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Kanuni ya Bunge ya 39(1) na 39(9). Kwa mujibu wa jibu la Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Na kwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais yupo

hapa Bungeni na Ofisi yake inahusika. Kwa nini usitoe idhini kwa mujibu wa ile Kanuni niliyoitaja ili aweze kutujibu kwa nini Wabunge hatuna taarifa na hatuhusishwi?

SPIKA: Makamu wa Rais hapa yupo kwenye *capacity* yake kama Mbunge. Kwa hiyo usije ukadandia vitu vingine.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka kutoa ufafanuzi tu kwamba Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar hayupo hapa Bungeni. Ambaye yupo hapa ni Mheshimiwa Seif Ali Idd ambaye ni Mbunge.

Kwa hiyo, kumtaka kwa kweli Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kujibu utakuwa unafanya jambo ambalo ni tofauti kidogo. Lakini suala la msingi hapa ni kwamba *TASAF* inasimamiwa na Ofisi ya Rais ambayo ni Ofisi ya Muungano, hilo la kwanza.

Lakini la pili, Kamati ya Sheria na Katiba inasimamia miradi yote ya Ofisi ya Rais, iwe inafanya kazi Bara au Visiwani. Kwa hiyo, Kamati hii inahusishwa na inaweza vilevile ikatembelea miradi na kudai maelezo yote yanayohusiana na utekelezaji wa *TASAF* Zanzibar.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge Kanuni anayoisemea Mheshimiwa inasema hivi “Waziri anaweza kuulizwa maswali kuhusu masuala yoyote ya Umma au jambo lingine lolote ambalo linasimamiwa na Ofisi yake.

Vilevile anaweza kuulizwa maswali kuhusu mambo yote anayohusika nayo kutokana na kuteuliwa na Bunge kushughulikia mambo hayo. Kwa hiyo, Makamu wa Rais

hajateuliwa na Bunge kushughulikia mambo ya *TASAF. (Makofi/Kicheko)*

Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 19

Madai ya Mafao Kwa Waliokuwa Wafanyakazi wa Kiwanda cha Nguo cha Morogoro (Morogoro Polytex)

MHE. MARGARETH A. MKANGA (K.n.y. ABDULAZIZ M. ABOOD) aliuliza:-

Kuna wafanyakazi 1,267 waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha *Polytex* mwezi Julai, 1997 wanadai mafao yao ambayo ni mshahara wa mwezi Desemba, 1998, kiinua mgongo, malipo ya likizo na gharama za usafirishaji mizigo lakini mpaka sasa wanayumbishwa na *Consolidated Holdings* hawajalipwa mafao yao:-

Je, ni lini wafanyakazi hao watalipwa haki zao wanazodai?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdulaziz Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Desemba 1998, Serikali kupitia iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* ambayo majukumu yake hivi sasa yamehamishiwa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma *(CHC)* ilisitisha ajira za wafanyakazi 1,124 wa iliyokuwa *Morogoro Polyster Textile Limited.*

Mwezi Desemba, 1998 wafanyakazi wote wapatao 1,124 walilipwa jumla ya shilingi 1,453,454,739 kama mafao yao ya kisheria ambayo yalijumuisha mshahara wa mwezi mmoja baada ya notisi na malimbikizo ya mishahara ya nyuma, malipo ya likizo, nauli ya mfanyakazi, familia na gharama za kusafirisha mizigo yao hadi makwao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumalizika kwa zoezi hilo Serikali ilipokea malalamiko ya madai ya baadhi ya wafanyakazi wakidai kupunjwa mafao yao katika baadhi ya maeneo. Malalamiko hayo yaliwasilishwa Serikalini kupitia iliyokuwa Menejimenti ya uangalizi yaani *(Caretaker team by then).* Madai yao yalijumuisha mshahara wa mwezi Desemba, 1998 kwa mantiki kuwa waliachishwa kazi Desemba 1998, lakini mafao yalilipwa hadi mwezi Novemba, 1998. Mapunjo kwenye malipo ya likizo, nauli, pamoja na mizigo.

Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kupokea malalamiko ya wafanyakazi hao ilifanya uhakiki ambapo jumla ya wafanyakazi 101 walilipwa mwezi Mei, 2011 baada ya kuwasilisha vielelezo vya madai ya mapunjo ya mishahara notisi ya kuachishwa kazi, likizo, nauli na mizigo.

Aidha madai ya kiinua mgongo hayakulipwa kwa sababu hayakuwa sehemu ya mafao ya kisheria wakati wanaachishwa kazi mwezi Desemba 1998. Baada ya malipo hayo mwezi Mei, 2011 wafanyakazi 1,183 waliwasilisha tena madai yao Serikalini ambapo yalipitiwa na kubainika kuwa hayakuwa na vielelezo vya kutosha kuwezesha kulipwa tena.

Kutokana na mapungufu yaliyojitokeza katika nyaraka za madai yao Serikali imeiagiza *CHC* kupitia upya madai ya wafanyakazi hao ambapo zoezi la uhakiki wa nyaraka linatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba 2012 na matokeo ya uhakiki huu utasaidia Serikali kufanya maamuzi juu ya madai hayo. *(Makofi)*

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa vile *CHC* imekwamisha malipo stahili ya wafanyakazi waliokuwa *NAFCO,* Mbarali na Kapunga hata baada ya kushinda kesi yao Mahakamani.

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya stahili za wafanyakazi hawa ambao wanadai lakini bila ya mafanikio?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): Mheshimiwa Spika, *CHC* haijakwamisha mafao ya

wafanyakazi waliokuwa *NAFCO.* Kinachofanyika hapa ni kwamba malalamiko yoyote lazima yafanyiwe uhakiki na sisi Serikali tunasubiri maelekezo ya matokeo ya uhakiki huo ambao *CHC* inafanya ili tuweze kulipa.

Malipo yanakuwa hayatolewi tu kwa utaratibu lakini inabidi lazima tuyapange katika bajeti na kuendelea kulipa. Kwa hivyo kama *CHC* nina hakika kwamba bado wanaendelea kufanya huo uhakiki ina maana tu itakapomaliza watatuletea sisi Wizara ya Fedha kwa ajili ya kufanya malipo.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Wafanyakazi wanaoidai Serikali kwa sababu ya kutokulipwa haki zao mbalimbali haiko kwa Kiwanda cha *Polyster* cha Morogoro peke yake, lakini yako maeneo mbalimbali nchini na ziko taasisi na Idara mbalimbali za Serikali. Je, Serikali inatoa tamko gani madhubuti kuhakikisha kwamba malalamiko yanayotolewa na wafanyakazi hao wengi wakiwepo wale wa Afrika Mashariki, *TAZARA, NAFCO* na taasisi nyingine ni lini sasa Serikali itahakikisha kwamba inalipa mafao na inaondokana na malalamiko ya wafanyakazi wa namna hiyo?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Zambi, ni zuri. Lakini ni vigumu kujibu kwa ujumla kwa sababu kila swali au kila jambo lina sababu yake ya kuchelewa. Kwa hivyo *CHC* kwa utaratibu ipo

kisheria, kanuni na taratibu zilizopo za kuchambua na kufuatilia tatizo kama lilivyo wanafanyakazi kama ipasavyo, kitu kikubwa tunachoomba wawe wanaharakisha katika kila jambo. Lakini kusema hapa Bungeni kwamba matatizo yote yanayoletwa yatatatuliwa lini, yanafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni. *(Makofi)*

Na. 20

Fedha Zilizorejeshwa Hazina

MHE. KABWE Z. ZITTO aliuliza:-

Katika mwaka wa Fedha 2010/2011, Wizara ya Fedha kupitia barua yenye Kumb. Na. EB/AG/40/0/Vol.5/003 iliagiza jumla ya Shilingi Milioni 175 za Kitanzania zirejeshwe Hazina kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma; ufuatiliaji unaonyesha kuwa Halmashauri zote nchi nzima ziliagizwa kurejesha fedha kwa mtindo huo ambapo miongoni mwa fedha zilizorejeshwa ni kwa Shule za Msingi na Sekondari:-

(a) Je, Wizara ya Fedha ilikusanya jumla ya fedha kiasi gani kutoka Halmashauri zote nchini?

(b) Je, fedha hizo zilitumika kwa shughuli gani?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto,

Mbunge wa Kigoma Kaskazini, yenye sehemu (a) na (b) kwa ujumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Agosti, 2011 ilibainika kuwa fedha za matumizi ya kawaida *(OC)* za mwezi zilizotumwa kwenye Halmashauri zilizidi kiasi kilichokuwa kimeidhinishwa na kikao cha *Resources and Expenditure Ceiling Committee* ya Wizara ya Fedha. Katika kikao hiki jumla ya sh. bilioni 12 ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwenye Halmashauri zote nchini.

Aidha, katika kipindi hicho Wizara ya Fedha ilipokea maombi ya ziada nje ya Bajeti kutoka kwenye Halmashauri kwa ajili ya zoezi la usimamiaji mitihani ya Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa fedha hizo zilizofikia bilioni 30 zikiwemo zile za ziada ilibainika kuwa kulikuwa na upungufu wa fedha za matumizi kwa ajili ya Mikoa na Wizara hivyo kulazimu Hazina kuwaandikia barua yenye Kumbukumbu Na. EB/AG/40/01/Vol.5/003 Wakurugenzi wa Halmashauri za Tanzania Bara ili kurejesha fedha hizo zisizozidi Mfuko Mkuu ili ziweze kutumika kwa shughuli nyingine ambazo zilikusudiwa.

Aidha, katika kutekeleza agizo hilo jumla ya Halmashauri 38 zimerejesha fedha zilizozidi kama walivyotakiwa kufanya ikiwemo vilevile Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.

Mheshimiwa Spika, katika zoezi hilo jumla ya Shilingi bilioni 4.3 zilirejeshwa Mfuko Mkuu na fedha hizo zilitumika

katika utaratibu wa kawaida wa utoaji fedha kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Hali kadhalika jumla ya Halmashauri 95 ambazo zilishindwa kurejesha fedha zilizozidi Wizara iliamua kuwakata kwenye migao yao ya miezi iliyofuata ambapo zoezi hilo lilikamilika mwezi Juni, 2011.

MHE. KABWE. Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, suala ambalo Mheshimiwa Waziri amelijibu la mwaka wa fedha 2011/2012. Kwa sababu mwezi Agosti, 2011 ambapo jibu linaonyesha ni mwaka mpya wa fedha kwa 2011/2012. Swali langu la mwaka wa fedha 2010/2011 ambao mwaka wa fedha unaitwa Juni 2011, kwa hiyo swali halijajibiwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, jumla ya shilingi trilioni 9 zilitolewa na Hazina kwenda kwenye Wizara, Mikoa na Halmashauri za Wilaya. Lakini taarifa ya *CAG* haionyeshi zaidi ya shilingi bilioni 25 ambayo kutokana na barua hii ambayo Hazina iliandika zilirudi Hazina na zilitumika namna gani. Sasa swali.

Serikali ipo tayari kufanya ukaguzi maalum wa fedha hizi ili kuweza kuhakikisha kwamba fedha za Umma zinatumika sawa sawa hasa ukizingatia kwamba Naibu Waziri amejibu mwaka wa fedha ambao sio swali lililoulizwa?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Kabwe Zitto. Suala lake kama linahusu mwaka wa fedha 2010/2011 tunalipokea kwa ajili ya uchunguzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 21

Hali Duni za Maisha Kwa Wanawake wa Bukombe

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI aliuliza:-

Pamoja na juhudi zilizofanywa na Serikali na wananchi za kuwainua wanawake kimaendeleo hapa nchini, wanawake wa Bukombe bado wana hali duni:-
(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wanawake wa Bukombe ili wajikwamue kutoka kwenye hali zao duni?

(b) Je, ni kwa nini siku hizi Bukombe haipati fungu la Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake?

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri, Mwenyekiti wa UWT Taifa (CCM). *(Makofi)*

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali naomba nichukue nafasi kidogo kwanza kuwapongeza wanawake wote wa UWT kwa kufanikisha chaguzi mbalimbali katika ngazi mbalimbali.

Aidha na mimi naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa kuonyesha imani kwangu na kunichagua kushika tena nafasi ya Uenyekiti wa UWT Taifa. Nawashukuru sana kwa kura nyingi zilizonipa ushindi wa kishindo kwa kupata kura nyingi walizopiga kura za kimbunga cha tsunami. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nimjibu Mheshimiwa Profesa Kulikoyela K. Kahigi, swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Kahigi kuwa Serikali imekuwa ikiwawezesha wanawake wa Bukombe kiuchumi ili waweze kujikwamua katika hali duni kwa kuwapatia mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF).*

Aidha, kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri, wanawake wamekuwa wakihamasishwa kujiunga na vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa yaani *SACCOS* pamoja na *VICOBA.*

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Bukombe haijapatiwa fedha za Mfuko kwa vile Halmashauri ya Bukombe haijarejesha Shs. 4,000,000/= walizopatiwa mwaka 2006. Hivyo namwomba Mheshimiwa Kahigi kwa vile wewe ni Mjumbe wa Kamati ya Mikopo ya Halmashauri ya Bukombe, ahimize Halmashauri kurejesha fedha hizo ili waweze kupatiwa zingine.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa nasikitika kwamba swali langu halikujibiwa vizuri. Niliuliza kuhusu mpango na mpango huo uwe endelevu na jumuishi.

Kama ni mpango unaohusu maendeleo ya kinamama na kujumuishwa na wanawake wote na siyo miradi au mipango midogo midogo ambayo inalenga wanawake wachache tu kama Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake shilingi 4,000,000/= zitawafikia wangapi?

Je, sasa hivi Serikali iko tayari kuangalia upya mipango hii iliyopo au miradi hii uliopo kwa ajili ya akinamama ili ufanywe kuwa endelevu na ijumuishe wanawake wote? Hilo swali la kwanza.

La pili, kuhusu fedha hii ambayo anasema kwamba haijarejeshwa shilingi milioni nne, Serikali ina mpango gani kuhusu Halmashauri ambazo hazirejeshi hizo fedha? Kwa sababu jambo hili limetokea mwaka 2006 mpaka sasa halijatatuliwa na hii fedha ilikuwa ni fedha ya umma na inawezekana hii fedha ilitafunwa tu. Sasa Serikali ina mpango gani kuwepo hizi Halmashauri? Ahsante sana.

SPIKA: Haya Mheshimiwa Waziri, lakini kujibu amejibu vizuri. Maana yake nimesoma hili swali nikaona limejibiwa kama alivyotaka.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, anazungumzia kuhusu kuwa na Mpango wa kuwaendeleza wanawake wote. Kwanza ningependa nimfahamishe kwamba katika kila Halmashauri Serikali Kuu ina Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri. Kwa hiyo, tunategemea kila Halmashauri iwe na mipango yake ya kuwaendeleza wanawake na watoto. Hatuwezi tukaweka mpango mmoja ambao unaweza uka-*fit* Dar es Salaam na uende uka-*fit* Katavi au Bukombe.

Kwa hiyo, kwa kupitia yeye nashauri kwamba sisi Wabunge ambao pia tupo katika ile Kamati ya kutoa mikopo na pia katika Kamati ya Fedha tukae tupange tuone kwamba tunafanyaje, kila Halmashauri iwe na mpango kwa ajili ya vijana na wanawake.

Pia, Serikali moja ya mpango wake ni katika uanzishwaji ule wa Benki ambao tunajitahidi kuwe na *Branch* sehemu nyingine. Lakini pia Serikali imewezesha taasisi mbalimbali za kifedha kuanzishwa ili waweze kukopesha wanawake sehemu mbalimbali nchini, imeweka mazingira mazuri ya kuwezesha vyombo hivyo kuweza kukopesha wanawake, vijana na watu wengine mbalimbali.

Swali lake la pili anauliza Halmashauri ambazo zimeshindwa kurudisha. Sababu ya kutaka zile fedha zirudishwe ni kuonyesha kwamba je, Halmashauri hii itasimamia ule mkopo, inakopesheka.

Suala kubwa hapa ni kujifunza utamaduni wa kukopesheka na ndiyo maana zilitolewa zile shilingi 4,000,000/= kama ni chachu. Iliyobakia ni kwamba kila Halmashauri itoe asilimia 5 ya mapato yake kwa ajili ya kukopesha wanawake na asilimia tano kwa ajili ya vijana. Hilo nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tulisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze sana Kamati ya *LAAC* ambayo kila inapoenda kwenye Halmashauri inaulizia hili kwanza, ni muhimu sana. Ahsante Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Na. 22

Chuo cha Waandishi wa Habari Tanzania

MHE. RASHID ALI ABDALLAH aliuliza:-

Tanzania ina Chuo cha Waandishi wa Habari na lengo kubwa ni kutoa taaluma juu ya uandishi wa habari ulio bora nchini:-

(a) Je, ni wanafunzi wangapi wanamaliza mafunzo hayo kila mwaka?

(b) Je, ni Waandishi wa Habari wangapi wanaoajiriwa na Serikali?

(c) Je, Waandishi wa Habari wangapi wameajiriwa na Serikali na hatimaye kuacha kazi?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania inavyo vyuo zaidi ya vinane vinavyofundisha taaluma ya Habari na Mawasiliano ya Umma, ambavyo vinatambuliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE).* Kati ya vyuo hivyo, vimo Vyuo Vikuu vinne ambavyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,

Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine, Chuo Kikuu cha Tumaini na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Vyuo vingine ni vile vinavyotoa mafunzo katika ngazi ya Cheti na Stashahada.

Aidha, Serikali inacho chuo kimoja kinachofundisha taaluma ya Habari na Mawasiliano ambacho ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Slaam. Awali, chuo hiki kilijulikana kama *Tanzania School of Journalism (TSJ),* kilichokuwa kikitoa mafunzo haya katika ngazi ya Stashahada na baadaye kuitwa Taasisi ya Habari na Mawasiliano ya Umma, iliyokuwa ikitoa mafunzo ya Stashahada ya Juu na Shahada. Kuanzia mwaka 2002 chuo hiki kiliunganishwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuitwa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma ambapo hadi sasa kinatoa mafunzo katika ngazi ya Shahada na Shahada ya Uzamili.

(a) Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi wanaomaliza mafunzo kila mwaka nchini ni kubwa. Mathalani, katika Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma wastani wa wanafunzi mia moja (100) wanamaliza masomo na kutunukiwa Shahada na Stashahada zao kila mwaka kuanzia miaka ya 2002/2003 hadi 2011/2012.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeajiri Waandishi wa Habari zaidi ya mia tatu (300) wanaofanya kazi kama Maafisa Habari na Mawasiliano katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mamlaka, Wakala na Taasisi mbalimbali za Serikali.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo, idadi ya Waandishi wa Habari wanaojiriwa na Serikali na hatimaye kuacha kazi Serikalini bado ni ndogo sana. *(Makofi)*

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nina masuala mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, viko vyombo vya habari vinawatumia Waandishi zaidi ya miaka miwili bila ya kuwaajiri. Je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya suala hili?

Swali langu la pili. Waandishi wetu wa Habari wanafanya kazi katika mazingira magumu na ya hatari. Hivi karibuni baadhi ya Waandishi wa Habari wameuawa. Mishahara yao ni midogo sana hailingani na kazi wanazozifanya.

Je, kuna hatua gani ya Serikali ya kuweza kuzingatia kwa nyongeza ya mishahara na posho zao? Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wapo Waandishi ambao wanafanya kazi katika vyombo vya habari ambao wanaweza wakakaa zaidi ya miaka hata miwili bila kuajiriwa.

Wito tu wa Serikali ni kwamba wapo Waandishi wanaofanya kazi katika Serikali na wapo wanaofanya kazi katika vyombo binafsi. Nitoe wito tu kwa watu wote

wanaoajiri Waandishi wa Habari kuzingatia kwamba wanawaajiri kufuatana na taratibu na sheria za kazi.

Pili, ni kweli mazingira ya kufanya kazi kwa Waandishi wa Habari bado si ya kuridhisha sana na ndiyo maana Serikali kwa nia nzuri inakuja na Muswada wa Habari utakaowasilishwa katika Bunge linalofuata.

Lakini pia ni kwamba mishahara midogo inategemea na makubaliano kati ya mwajiri na mwajiriwa na hawa ni Waandishi walioko Serikalini na wengine katika vyombo vya watu binafsi. Nitoe wito tu kwamba vyombo vile vikae na mvione kwamba vinatoa maslahi mazuri kwa ajili ya Waandishi wa Habari na kufanya kazi katika mazingira mazuri zaidi. *(Makofi)*

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, mbali na kwamba Waandishi wa Habari waliokuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu ikiwepo kulipwa malipo madogo na hasa wale wa *Correspondent* pamoja na walioajiriwa.

Lakini pia kuna tatizo kubwa sana ambalo linachangia Waandishi wa Habari kutoa habari bila ku-*balance.* Katika Serikali na hasa kwenye Wizara kushindwa kutoa habari kwa Waandishi wa Habari pale ambapo zinapohitajika wakati hii ni haki ya msingi ya vyombo vya habari kupata taarifa.

Sasa je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inatoa ushirikiano kwa vyombo vya habari pale inapohitaji taarifa kwa maslahi ya Umma?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Waandishi wengine wanaandika habari bila ya ku-*balance* hizo habari. Nitoe wito tu kwamba wazingatie maadili ya Uandishi wa Habari na kuona kwamba wana-*balance* hizo *story* zao.

Lakini lingine ni kwamba Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kupitia Maafisa Habari katika Wizara kuona kwamba habari zinazohitajika katika Wizara mbalimbali, katika Serikali zinapatikana kwa wakati. *(Makofi)*

SPIKA: Tuendelee kwa sababu ya muda Waheshimiwa tuna maswali manane tu tumeyajibu tunapaswa kujibu maswali kumi kwa sasa. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Yusuf A. Nassir, atauliza swali hilo.

Na. 23

Jengo la Kiwanda cha Matunda Korogwe

MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI (K.n.y. MHE. YUSUPH A. NASSIR) aliuliza:-

Kilichokuwa kiwanda cha Matunda Korogwe kiliwahi kutoa ajira kwa Wananchi wa Korogwe wakiwemo wakulima wa matunda aina ya machungwa na maembe:-

Je, Serikali inasemaje kuhusu hatima ya jengo la kiwanda hicho ambalo bado lipo?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yusuph Abballah Nassir, napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1992 Viwanda vya Matunda ya TANGOLD Dar es Salaam na TANGOLD Korogwe vikiwa chini ya kampuni tanzu ya Shirika la Usagishaji la Taifa *(NMC)*, vilikodishwa kwa Kampuni ya *Noble Azania Investment and Management Services* kwa kipindi cha miaka kumi.

Mkodishaji alikiuka masharti ya Mkataba ambapo pamoja na mambo mengine, alibadili jina la Kampuni ya TANGOLD kuwa *Noble Food Beverages Ltd.* na kuhamisha mitambo kutoka kiwanda cha Korogwe kupeleka kwenye kiwanda cha Dar es Salaam.

Mwaka 1998, *NMC* iliainishwa, yaani kuwa *specified* ili kubinafsishwa na mkodishaji alitakiwa kukabidhi mali hizo kwa Serikali kwa ajili ya kubinafsishwa. Mkodishaji aliamua kwenda Mahakamani kuweka zuio, yaani *Court Injunction Order,* kwa ajili ya kiwanda cha TANGOLD Dar es Salaam, ambacho bado mpaka sasa kina kesi Mahakamani.

Iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma, yaani *PSRC*, ilichukua Kiwanda cha TANGOLD Korogwe ambacho hakina kesi na kilikuwa kimetelekezwa na kuwa katika hali ya kutoridhisha kwani vifaa vingi

vilihamishwa na vingine viliibiwa na hivyo kubaki jengo tu. *PSRC* walitangaza kuuza kiwanda hicho kwa nyakati mbalimbali na hawakuweza kupata mnunuzi mwenye sifa zilizohitajika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nassir, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Korogwe na Muheza ni maeneo ya kimkakati kwa uzalishaji wa matunda, Serikali imeamua kutumia utaratibu wa ubia, yaani *Public Private Partnership,* kuendeleza usindikaji wa matunda katika jengo la kiwanda hicho. Kwa sasa Serikali inafanya utaratibu wa kukabidhi majengo ya kiwanda hicho kati ya Mamlaka ya Mauzo Nje ya Nchi, yaani *EPZA* au Kituo cha Taifa cha Uwekezaji *(TIC),* kulingana na matokeo ya mipango yao ya kukiendeleza kiwanda hicho kwa kushirikiana na wawekezaji.

Tayari Serikali imepokea programu za majaribio za kuwekeza na kusindika matunda katika kiwanda hicho toka *EPZA* na *TIC* na kikao cha kutoa maamuzi ya nani akabidhiwe kiwanda kitafanyika hivi karibuni.

MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Katika jibu lake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Wilaya ya Korogwe na Muheza ni maeneo ya kimkakati. Je,

Waziri atakubaliana na mimi kwamba kwa vile Wilaya ya Lushoto nayo inazalisha matunda kwa wingi hasa *apples, plums* na *peas* nayo iorodheshwe katika maeneo ya kimkakati?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa kifupi, Wilaya ya Lushoto na maeneo yote ambayo yanalima matunda, ambayo mara kwa mara tukipita tunaona yanaoza, yote tumeyajumuisha katika maeneo ya kimkakati. Kwa hiyo, sasa hivi tuna utaratibu, kupitia *NGO* yetu ya *TAHA* tumeandaa mpango mzuri kabisa ambao utashirikisha Wilaya zote au maeneo yote yanayolima matunda ili tuweze kuendeleza mazao yote ya matunda kwa mpango wa *horticulture development*. Kwa hiyo, Lushoto nayo imo katika maeneo ya kimkakati.

SPIKA: Ahsante, kwa sababu ya muda tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi.

Na. 24

Reli ya Manyoni – Singida Kutokufanya Kazi

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA (K.n.y. MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI) aliuliza:-

Reli ya Manyoni - Singida iliyojengwa miaka ya hivi karibuni haijawahi kufanya kazi kwa ufanisi na hivi sasa haitumiki:-

(a) Je, Serikali itakubali kuwa reli hiyo ilijengwa bila tathmini ya kina juu ya mahitaji yake?

(b) Je, ni hasara kiasi gani imepatikana kila mwaka kutokana na reli hiyo kutofanya kazi na miundombinu yake kuharibika?

WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Reli ya Manyoni - Singida ilijengwa kutokana na kuwepo kwa mahitaji makubwa ya kusafirisha shehena za mizigo kutoka katika mashamba makubwa ya ngano yaliyopo Basutu, pamoja na kutoa huduma ya usafiri wa abiria kati ya Manyoni na Singida. Kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2005, wakati reli hiyo ilipokuwa chini ya usimamizi wa Serikali, ilikuwa ikisaidia kutoa huduma ya usafiri wa reli katika eneo hilo.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali ilifanya tathmini ya kina kabla ya kujenga reli ya Manyoni kwenda Singida. Aidha, kutokana na miundombinu ya barabara katika maeneo hayo kwa kipindi hicho kutokuwa katika hali nzuri na kusababisha tatizo la upatikanaji wa huduma nzuri ya usafiri, kulichangia kuwepo kwa umuhimu wa kujenga reli hiyo.

Mheshimiwa Spika, huduma za usafiri wa reli kati ya Manyoni na Singida zilianza kusuasua na hatimaye kusitishwa mwaka 2007 wakati Shirika la Reli Tanzania *(TRC),* lilipokodishwa kwa Kampuni ya RITES kutoka India, Kampuni ambayo haikutoa umuhimu kwa sehemu hiyo ya reli. Hata hivyo, Kampuni hiyo ilishindwa kuendesha Shirika hilo na hatimaye Shirika hilo lilirudishwa Serikalini.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inapata hasara zifuatazo kutokana na Reli ya Manyoni – Singida kutofanya kazi; kwanza, kukosa mapato yatokanayo na usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia za reli zilizofungwa; pili, kuingia gharama kwa kufanya ukaguzi wa njia za reli zilizofungwa kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati pindi fedha zitakapopatikana na kuhakikisha kuwa haziendelei kuharibika zaidi; na tatu, kuingia gharama za kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara barabara kutokana na barabara hizo kuharibika kwa sababu ya kupitisha magari yanayobeba mizigo mizito kwa umbali mrefu ambapo mizigo hiyo ilitakiwa isafirishwe kwa njia ya reli.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Katika Mkutano wa Pili wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaani Bunge la Februari, 2011, mimi mwenyewe niliuliza swali kuhusu Reli hii ya Manyoni – Singida kwamba ni lini itafufuliwa kutokana na matatizo haya ambayo pia Waziri ameyaorodhesha hapa. Aliyekuwa Naibu Waziri kwa wakati ule Mheshimiwa Mfutakamba alijibu kwa uhakika kwamba Reli ile ya

Manyoni – Singida ingefufuliwa baada ya kutengewa bajeti ya mwaka 2011/2012 lakini mpaka sasa sikuona chochote ambacho kimefanyika.

Swali langu ni kwamba ni kwa nini Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Serikali alitoa ahadi ambayo haikuweza kutekelezwa mpaka sasa na kuwapa matumaini hewa Wananchi wa Mkoa wa Singida?

(ii) Kwa kuwa Mkoa wa Singida unakua kwa kasi na unaendelea kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji ikiwemo uzalishaji wa alizeti na ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kuku na vyote hivi kwa pamoja vinategemea kwa kiasi kikubwa usafiri wa reli na reli inayotegemewa ni ya Manyoni – Singida. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuifufua reli hii ili iweze kuongeza kipato cha Wananchi wa Mkoa wa Singida na pato la Taifa kwa ujumla?

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nisisitize kwa Mheshimiwa Mbunge kwamba, ahadi zinatekelezwa kwa fedha na sijui kama Mheshimiwa Mbunge ana kumbukumbu yoyote ya kwamba fedha ilitengwa kwa ajili ya ukarabati wa reli hiyo. Mimi ninavyojua fedha haikutengwa.

Pili, naomba nimhakikishie kwamba tayari wataalam katika Wizara yangu wanaikagua reli hii kwa lengo la kuifanyia ukarabati. Tunachomwomba Mheshimiwa Mbunge, atuunge mkono tutakapokuja hapa na Bajeti halisi kwa ajili ya reli hiyo.

Na. 25

Usalama wa Wasafiri Majini

MHE. JUMA SURURU JUMA aliuliza:-

Hapa nchini kumetokea matukio ya ajali kubwa za baharini na Maziwani kama vile kuzama kwa meli za MV-Skagit, MV Spice Islanders na MV Bukoba na kugharimu kwa kiasi kikubwa maisha ya wananchi na maiti nyingi kushindwa kutolewa ndani ya maji. Hivi sasa wananchi wana mashaka juu ya uwezo wa Serikali katika kukabili majanga haya:-

Je, Serikali inawahakikishia nini Watanzania kuhusu usalama wa maisha yao kwa wasafiri wa majini?

WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Jimbo la Bububu, kama ifuatavyo:-

Serikali inaendelea kuimarisha usalama wa usafiri majini ili kuepuka ajali na matukio mbalimbali yanayoathiri maisha ya watu na mali. Baada ya ajili ya MV Spice Islanders na MV Skagit, Serikali imeendelea kutathmini upungufu uliopo katika sekta na kutafuta ufumbuzi ambao utatusaidia kuepukana na ajali kama hizi kutokea hapo baadae. Baadhi ya hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali ni pamoja na kutengeneza Kanuni za kuimarisha udhibiti wa vyombo vya usafiri majini na usalama wa abira na mali zao,

kufanya kaguzi mara kwa mara kwa vyombo vya majini ili kubaini ubora wake, kutoa elimu kwa wananchi ili kujua wajibu wao wa kujilinda wanapokuwa safarini, kutoa elimu kwa wamiliki na wafanyakazi melini kuwa na maamuzi sahihi wawapo safarini kwa kuzingatia taarifa za hali ya hewa na wajibu wao kwa maisha ya abiria waliowabeba kwenye vyombo vyao, taratibu za kuruhusu meli kuondoka bandarini zinapewa umuhimu mkubwa na kusimamiwa na mamlaka za kudhibiti usalama na usafiri wa majini na nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha shughuli za kukabiliana na majanga hayo, Serikali imeandaa Muswada wa Sheria kuhusu utafutaji na uokoaji katika usafiri wa majini na wa anga kwa pamoja. Hii ni kutokana na miongozo ya utafutaji na uokoaji iliyotolewa na Mashirika ya Kimataifa ya Usafiri Majini *(IMO)* na Usafiri wa Anga *(ICAO).*

Muswada huu wa Sheria unategemea kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari mwaka kesho. Sambamba na Muswada huo, pia umeandaliwa Mpango wa Taifa wa Utafutaji na Uokoaji utakaotumika kutoa mwongozo wa shughuli za utafutaji na uokoaji nchini.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na maandalizi ya Muswada na Mpango Mkakati; je, kuna mpango gani wa dharura wa uokoaji iwapo itatokea ajali hiyo kwa kipindi hiki?

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imechukua tahadhari kubwa sana kuhakikisha kwamba ajali ya aina ile haitokei tena. Viongozi Waandamizi wa nchi yetu walituamuru sisi Mawaziri katika Wizara zinazohusiana na usimamizi wa usafiri majini, kukutana kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuweza kuoanisha taratibu na Sheria za kuweza kudhibiti usalama wa vyombo vya majini.

Tumeshakutana na ninakuhakikishia kwamba, tumeongeza kasi na bidii ya kukagua vyombo hivi vya usafiri majini na vilevile tumekubaliana kuhakikisha kwamba hatusajili meli yoyote ambayo ina umri wa zaidi ya miaka 15 kwa usajili wa kwanza.

Hatua hizi tulizozichukua zinahakikisha kwamba hatutakuwa na ajali kama hiyo. Pindi matatizo yatakapotokea, tumejipanga vizuri, siyo tu sisi peke yetu, pamoja na Vyombo vingine vya Taifa ambavyo viko majini. Kwa mfano, Jeshi la Wananchi na Majeshi mengine kama vile KMKM na kadhalika.

SPIKA: Tuendelee, muda umebaki kidogo, swali linalofuata ni la Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe atauliza swali hilo.

Na. 26

Kusambaza Umeme katika Wilaya ya Serengeti

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE (K.n.y. MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE) aliuliza:-

Mwaka 2011 Serikali iliahidi kutenga shilingi bilioni 3.3 kwa ajili ya kusambaza umeme katika Wilaya ya Serengeti:-

(a) Je, Serikali imepanga kufanya nini kwa mwaka huu wa fedha juu ya ahadi hiyo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza nguvu ya umeme kwa maeneo yenye *single phase* na kuwa *three phase* na kuweka transfoma maeneo ya Burunga, Nyakiitoa, Bwitengi na sehemu nyingine?

(c) Je, kuna mpango gani umeandaliwa wa kusambaza umeme katika vituo vya kutolea huduma ya afya pamoja na Shule za Sekondari Wilayani Serengeti?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* na Wakala wa Nishati Vijijini, yaani *REA,* inaendelea kutekeleza Mpango wa Awamu ya Pili ya Kupeleka Umeme Vijijini Nchini chini ya Miradi ya *Turn-Key* katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. TANESCO imetenga jumla ya shilingi milioni 20.47 kwa ajili ya kubadilisha njia ya umeme kutoka *single*

phase hadi *three phase* ili kuboresha na kuongeza nguvu ya umeme katika eneo la Bwitengi kwa kuondoa transfoma ya KVA 25 ya *single phase* na kuweka ya KVA 50 ya *three phase*.

Mheshimiwa Spika, Mradi huo pia unahusisha ufungaji wa transfoma ya 50 KVA katika Kijiji cha Nyakitono na kusambaza umeme eneo hilo kwa gharama ya shilingi milioni 37.43. Maeneo mengine ambapo mifumo ya umeme itaboreshwa ni pamoja na Nyamoko, Bomani Misitu na Minadani Misitu, ambapo itagharimu shilingi milioni 111.27. Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini, itatumia Mfuko wa Nishati Vijijini kutekeleza Mradi wa Umeme katika Vijiji vya Masinki, Rung'abure, Msati, Iramba, Majimoto, Usawe, Unchanchari na Marasomoche. Mradi huo umepangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa msimamo wa Serikali ni kuhakikisha kwamba, Miradi yote inayotekelezwa inazingatia upitishwaji umeme katika sehemu za huduma muhimu za kijamii kama vile shule za msingi, sekondari, zahanati, pampu za maji na kadhalika kama sehemu ya Miradi ya Msingi.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongozakama ifuatavyo:-

(i) Kuna baadhi ya sehemu ambazo Mradi wa Umeme wa *REA* umeshatekelezwa, kwa mfano, katika

Wilaya ya Tarime, lakini haukupita katika sehemu za huduma muhimu kama shule za sekondari na vituo vya afya. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba maeneo ambayo yana umeme wa *REA* na sehemu ambazo zina shule ya sekondari na vituo vya afya vinapata umeme huo?

(ii) Mpango huo utatekelezwa lini katika Wilaya ya Serengeti?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kweli nikiri kwamba, katika miradi ya awali yapo baadhi ya maeneo ambako katika *design* ya miradi ile inayopeleka umeme vijijini, haikuzingatia sehemu muhimu za huduma za jamii kama sekondari, shule za msingi na zahanati au hospitali na maeneo mengine muhimu ambayo kwa mijini yakipata umeme yanakuwa yanasaidia sana jamii.

Wizara yetu imeiagiza *TANESCO* na Wakala wetu wa *REA*, kuhakikisha kwamba maeneo hayo sasa katika Miradi yote ambayo inafuata basi inazingatia maeneo hayo.

Huwezi kusema eti umeme umefika kwenye kijiji fulani, kama haujafika sehemu ya shule ya msingi, sehemu ya sekondari, kwenye zahanati na sehemu pampu ya maji, mimi nadhani hapo umeme unakuwa haujafika bado kwenye kijiji. Kwa hiyo, msimamo wa Serikali ni huo kwa Miradi yote inayoendelea.

Kuhusu tutafanya nini; ni kwamba, kwa kweli kwa sasa tuombe sana wadau wakiwepo Wananchi na Uongozi wa

Kijiji, lakini na Halmashauri zitusaidie katika kuhakikisha kwamba zinapeleka hasa umeme kwenye maeneo ya jamii. Nimesema Halmashauri lazima zichukue jukumu la umeme kama sehemu ya Miradi yake ya maendeleo. Serengeti ni lini? Basi ni wakati wowote Serikali itakapokuwa na fedha ya Miradi hii tutatekeleza lakini kama nilivyosema ile ya mwaka 2012/2013 itaanza kutekelezwa wakati wowote kuanzia sasa.

SPIKA: Ahsante, tuendelee na Wizara ya Ujenzi, swali litaulizwa na Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Ameir.

Na. 27

Kupunguza Ajali na Vifo katika Mji wa Mikumi

MHE. ABDULSALAAM SELEMANI AMEIR aliuliza:-

Mji Mdogo wa Mikumi unakua kwa kasi na kwamba barabara kuu iendayo Zambia inayopita katikati ya Mji huo husababisha kuwepo kwa ajali na vifo vingi vya wananchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza ajali kwenye barabara hiyo kwa kuweka matuta?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Ameir, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kiusalama ikiwemo uwekaji wa alama za barabarani za kupunguza mwendo katika eneo hili, lakini alama hizo zimekuwa zikiibiwa na zingine kugongwa na magari yanayoegeshwa kwenye eneo hilo. Madereva pia wamekuwa wakikiuka Sheria za Usalama Barabarani na kuendesha magari kwa mwendo kasi usioruhusiwa. Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuimarisha usalama wa watumiaji barabara katika eneo hili, kwa mwaka huu wa fedha wa 2012/2013, imepanga kuchukua hatua zifuatazo:-

Kwanza, kupanua maegesho ya magari pande zote za barabara katika Mji wa Mikumi ili barabara iwe wazi kwa magari yanayopita bila kusimama. Pili, kuongeza urefu wa barabara zinazoingia mzani wa Mikumi pande zote za mzani ili magari yanayoenda kupimwa yasisimame barabarani. Tatu, kuweka upya alama za barabarani zilizoharibiwa ili kupunguza mwendo kasi wa magari yanayoingia na kutoka Mji wa Mikumi. Nne, kuweka alama za barabarani kwa ajili ya vyombo vya moto pamoja na watembea kwa miguu.

Mheshimiwa Spika, zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo zipo kwenye hatua ya tathmini *(evaluation)* ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya kazi hizi. Kazi hizi zitaanza mara baada ya kumpata mkandarasi na zimepangwa kukamilika ndani ya Mwaka huu wa Fedha wa 2012/2013. Jumla ya shilingi bilioni 1.3 zimetengwa kwa ajili ya kazi hii.

MHE. ABDULSALAAM SELEMANI AMEIR: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri. Swali langu la msingi lilikuwa ni je, lini matuta yatawekwa katika Mji wa Mikumi katika barabara hiyo, kwa sababu kuanzia Dar es Salaam mpaka Mbeya, sehemu nyingi kwenye miji midogo wameweka matuta kwa ajili ya kuzuia ajali. Mikumi kila mara ajali hutokea kwa sababu hakuna matuta yanayozuia magari kwenda *speed.* Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie ni lini matuta yatawekwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kwenye jibu la msingi nimejaribu kuainisha kwamba, uwekaji wa matuta siyo *solution* ambayo itamaliza ajali. Kitu kikubwa hapa ni lazima kuzingatia Sheria na tumeainisha kwamba tunachukua hatua mbalimbali. Sasa pale ambapo tunaweza kuweka alama za kutosha, hakuna sababu ya kuweka matuta. Pale ambapo ni lazima tuweke matuta, tutaweka kwa kuzingatia vigezo ambavyo vinatakiwa na Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo, kwa jibu la msingi hili linatosheleza kabisa kuonesha hatua za kiusalama zimechukuliwa kuhakikisha kwamba ajali zitapungua katika eneo la Mji wa Mikumi.

Na. 28

Utoaji Hukumu kwa Lugha ya Kiswahili

MHE. SARA MSAFIRI ALLY aliuliza:-

Kesi katika Mahakama zetu nchini huendeshwa kwa Lugha ya Kiswahili lakini hukumu hutolewa kwa Lugha ya Kiingereza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hukumu zinatolewa kwa Lugha ya Kiswahili ili watuhumiwa wapate haki ya kujua hukumu zao kwa ufasaha?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA aliuza:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kupitia Mkutano wa Nane, Swali Namba 116 la tarehe 2 Julai, 2012 la Mheshimiwa Profesa Kahigi, Wizara yangu ilijibu swali kuhusiana na uandishi wa hukumu kwa Lugha ya Kiswahili. Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na kwa ridhaa yako, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, kesi nyingi katika Mahakama zetu nchini zinaendeshwa kwa Lugha ya Kiswahili lakini hukumu zinatolewa kwa Lugha ya Kiingereza. Utaratibu huu wa matumizi ya lugha mbili Mahakamani unafanyika kwa mujibu wa Sheria za nchi na Kanuni mbalimbali zinazoongoza mienendo na uandishi wa hukumu katika Mahakama zetu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11 kupitia kifungu cha 13(1) na (2), vinaeleza bayana kwamba, Lugha ya Mahakama ya Mwanzo itakuwa ya Kiswahili na Lugha ya Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi itakuwa ya Kiingereza au Kiswahili au Lugha yoyote ambayo Hakimu ataelekeza.

Aidha, Sheria hiyo inatamka bayana kwamba, kumbukumbu na hukumu za Mahakama za Wilaya na Mahakama za Hakimu Mkazi zitatakiwa ziwe katika Lugha ya Kiingereza.

Hata hivyo, kupitia Kanuni ya Pili ya Kanuni ya Lugha za Mahakama, Tangazo la Serikali Namba 31 la mwaka 1996 na Kanuni ya Tano ya Kanuni za Mahakama ya Rufani za Mwaka 2009 na Tangazo la Serikali Namba 368 la mwaka 2009, pia linatamka bayana kwamba, Lugha ya Mahakama itakuwa ni Kiingereza au Kiswahili lakini hukumu, amri au Maamuzi ya Mahakama yatatakiwa yaandikwe katika Lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa linalosababisha uandishi wa hukumu kuwa katika Lugha ya Kiingereza ni kutokana na masuala ya kisheria kuwa ya kiufundi na naamini sote tunatambua kwamba, istilahi mbalimbali za kisheria bado hatunazo nyingi na maamuzi mbalimbali ya kesi yamekuwa yakiangalia masuala mengine kama maamuzi mbalimbali ya kesi za nyuma.

Kwa hiyo, imekuwa ni vigumu kwa hivi sasa kuanza kutumia Lugha ya Kiswahili katika uandishi wa Hukumu.

Matumizi ya Lugha hizi Mahakamani yanatokana na utekelezaji wa Sheria za nchi na Kanuni zinazohusiana na Lugha ya Mahakama. Vilevile uamuzi wa kutumia Lugha ya Kiingereza katika uandishi wa hukumu na maamuzi ya Mahakama bado ni muhimu katika maamuzi ya baadhi ya kesi Mahakamani.

Hata hivyo, Serikali kwa kuona umuhimu wa kutumika kwa Lugha ya Kiswahili katika tasnia ya Sheria, inaendelea kutafsiri Sheria zake katika Lugha ya Kiswahili na inaangalia uwezekano wa kuona ni kwa namna gani sasa tunaweza tukaitumia Lugha ya Kiswahili katika uandishi wa hukumu lakini pia katika kumbukumbu za Mahakama.

MHE. SARA MSAFIRI ALLY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Kiswahili ndiyo Lugha ya Taifa na wananchi wengi wanaielewa; je, Serikali ipo tayari kushirikisha wadau mbalimbali kutoa maoni yao ili Sheria na Kanuni ambazo amezisema Mheshimiwa Waziri ziweze kujadiliwa na hatimaye ziweze kuletwa hapa Bungeni tuzifanyie marekebisho?

(ii) Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali inaendelea kutafsiri Sheria kwa Lugha ya Kiswahili; je, ni Sheria ngapi hadi sasa zimeshatafsiriwa kwa Lugha ya Kiswahili?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika swali la kwanza, ametaka kujua endapo Serikali ipo tayari kushirikisha wananchi na wadau mbalimbali, waweze kutoa maoni yao kuhusiana na Sheria hizi ambazo zinataka hukumu kuandikwa kwa Kiswahili.

Kwanza kabisa, suala hili ni pana na sidhani kama mjadala huu wa Kitaifa unatakiwa tu kuwa katika masuala ya uandishi wa hukumu bali naamini tunatakiwa tuanzie katika suala la mitaala na ni lugha gani ambayo tunaitumia katika kufundishia mashuleni.

Swali la pili ametaka kujua ni Sheria ngapi ambazo tumetafsiri hadi sasa. Itakuwa ni ngumu kumtajia idadi lakini katika mwaka wa fedha uliopita wa 2011, Julai, hadi sasa tumeshatafsiri Sheria 18 ikiwepo Sheria ya Maambukizi ya UKIMWI, Sheria ya Walemavu na Sheria zingine. Ahsante sana.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa ruhusa ili nimwulize swali dogo la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba sababu kubwa ambayo inapelekea hukumu kuwa katika lugha ya Kiingereza ni kwa sababu taaluma ya Sheria inahitaji istilahi za kiufundi. Nilikuwa ninahitaji pengine aweze kutoa ufafanuzi kigezo ambacho kimesababisha Wizara ya Sheria na Katiba kuweza kufikia uamuzi huo kwamba suala la matumizi ya Kiswahili tatizo ni uhaba wa istilahi za kiufundi, je, kuna utafiti wowote ambao wameufanya? Kwa sababu kwa uelewa wangu, ninatambua kuwa lugha ya Kiswahili imekuwa na ina msamiati wa kutosha, sioni tatizo kwamba kunakosekana istilahi ambazo zinaweza kuwa ni *common* katika kuandika hukumu kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, napenda atueleze kama wamefanya utafiti na kama utafiti huo umefanyika, je, Wizara au Serikali itakuwa tayari kuweza kutupatia tafiti hizo sisi Waheshimiwa Wabunge pengine kuweza kujiridhisha na kauli ambayo imetolewa na Serikali?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Machali anataka kujua ni sababu gani zinazopelekea kuandika hukumu kwa kutumia lugha ya Kiswahili na kama endapo Serikali imefanya utafiti, kwanza kabisa umefanyika utafiti lakini siwezi kusema kama ni utafiti rasmi lakini tafiti ni tafiti na baadaye atakapohitaji tutamletea matokeo ya tafiti hizo lakini Kiswahili kinachotumika katika uandishi wa hukumu ni Kiswahili kigumu na ninaamini hata Wabunge, siyo wengi ambao wana uwezo wa kufahamu Kiswahili kigumu. Lakini katika utoaji wa hukumu Mahakamani pamoja na kwamba hukumu zinaandikwa kwa lugha ya Kiingereza huwa Jaji au Hakimu anamsomea mtuhumiwa hukumu yake kwa kutumia lugha ya Kiswahili ili aweze kufahamu hukumu ilivyoandikwa. Ahsante.

SPIKA: Muda umekwisha, ninaomba tuendelee na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mheshimiwa Madabida ana tatizo la kiafya na swali hilo kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid.

Na. 29

Hospitali ya Lugalo kuwa Rufaa

MHE. NEEMA M. HAMID (K.n.y. MHE. ZARINA S. MADABIDA) aliuliza:-

Hivi karibuni Serikali ilipandisha hadhi Hospitali ya Jeshi ya Lugalo kuwa Hospitali ya Rufaa ambapo iliweza kusaidia kupunguza msongamano katika hospitali nyingine na kusaidia wakati wa mgomo:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani wataalam wa hospitali hiyo wana uelewa wa kutumia vifaa vya kisasa vya Hospitali ya Rufaa?

(b) Je, Serikali iko tayari kuipatia hospitali hiyo vifaa muhimu na kusomesha wataalamu wake?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba kutoa maelezo kuhusu Hospitali ya Jeshi la Lugalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Lugalo yenye vitanda 240 ndiyo hospitali kubwa ya Jeshi la Wananchi na imekuwa ikitumika kama hospitali ya Rufaa kwa hospitali nyingine za Jeshi.

Mwezi Novemba 2010, kwa Tangazo Na. 828 katika Gazeti la Serikali, hospitali hiyo ilipandishwa hadhi kuwa hospitali ya Kanda ya Mashariki ili itoe huduma za Kibingwa ngazi ya juu kwa Mikoa ya Kanda ya Mashariki (Morogoro, Pwani na Dar es Salaam). Mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Novemba, 2010 hospitali ilianza kutoa huduma za Kibingwa kama Hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Zarina Shamte Mdabida, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wataalam wa hospitali hiyo wamepata mafunzo katika vyuo vinavyotoa mafunzo kwa wataalam wote wa afya. Hospitali hiyo imekuwa ikitumika kutoa huduma za ngazi za rufaa kwa hospitali nyingine za Jeshi pamoja na za kiraia, hivyo hawa wataalam wana uelewa wa kutosha katika kutumia vifaa vya kisasa vya hospitali ya rufaa. Hata hivyo kama ilivyo kwa wataalam wengine kifaa kipya kinapoletwa inabidi wapate mafunzo ya namna ya kukitumia.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiipatia vifaa hospitali hiyo kila inapohitajika. Aidha, Serikali imekuwa ikitoa mafunzo kwa wataalam wa Hospitali hiyo kama inavyofanya kwa watumishi wa vituo na hospitali za umma. Aidha, wakati wa mgomo Serikali ilitoa dawa na vifaa

vyenye thamani ya shilingi 100,000,000 kuboresha huduma zilizotolewa katika hospitali hiyo. Bado Serikali itaendelea kuipatia dawa na vifaa zaidi na vya kisasa kadri bajeti itakavyokuwa ikiongezeka.

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili tu ya nyongeza.

Swali la kwanza, chumba cha kuhifadhia maiti cha hospitali ya Lugalo ni kidogo na kwa kuwa hospitali hiyo imepandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Rufaa, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa chumba hiki cha kuhifadhia maiti kinaboreshwa ili kiwe kikubwa kuweza kukidhi mahitaji?

Swali langu la pili ni kwamba tumeona kuwa hii Hospitali ya Lugalo mara nyingi inafanya kazi nyingi nzuri sana wakati wa dharura kwa mfano kipindi cha mgomo wa Madaktari, je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha zile hospitali zingine za jeshi zilizokuwa katika kambi mbalimbali hapa nchini katika Mikoa mbalimbali zinaweza kuboreshwa ili kuweza kukidhi mahitaji katika vipindi hivi vya dharura?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa hospitali hizi zote za Kanda na hospitali ile ya Taifa zipo chini ya Wizara ya Afya na kwa tafsiri hiyo tutaangalia namna ambavyo tutaweza kuboresha chumba hicho cha kuhifadhia maiti kutegemea na mahitaji na uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa hospitali za jeshi zote zilizoko nchini zinachangia sana katika kutoa huduma hata kwa raia na ni muhimu kuzipa nafasi yake ya kupata vifaa na wataalam ili ziweze kutoa huduma bora na nzuri kama zilivyo hospitali zingine za umma.

Katika mtazamo huo, bado Serikali itaendelea kutoa mchango wake kuhakikisha kuwa hospitali zote za Serikali na za jeshi zinaboreshwa ili ziweze kutoa huduma inayotarajiwa katika ngazi husika ya hospitali.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, pamoja na upungufu wa vifaa katika hospitali mbalimbali hapa nchini katika Bunge la Bajeti lililopita, Bunge lilipitisha zaidi ya shilingi bilioni 18 kwa ajili ya kulipa *On Call Allowances* kwa ajili ya Madaktari, lakini cha kusikitisha fedha hizo bado haziendi. Mfano ni katika hospitali ya Mgara pale Babati Madaktari hawajalipwa *On Call Allowances* kwa miezi mitatu, sasa ninapenda kufahamu kwa nini fedha hizo haziendi?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwanza suala tulilokuwa tunalizungumzia ni suala la hadhi ya hospitali ya Lugalo na swali la nyongeza linahusu *allowances,* lakini pamoja na hayo ni kweli kabisa kuwa Serikali ilitenga fedha shilingi bilioni 18 kwa ajili ya kulipa *On Call Allowances* kwa Madaktari wote nchini na kwamba upatikanaji wa fedha au upelekaji wa fedha katika Wilaya na Mikoa husika ndiyo unatarajiwa baada ya wao kupokea ndiyo watakuwa wanaendelea kulipa. Kwa hiyo, sina uhakika sawasawa juu ya hospitali hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge anaielezea lakini ninavyofahamu fedha hizo zitakuwa zinapelekwa katika Mikoa husika na

viongozi katika Mikoa ile wanawajibu wa kulipa kadri fedha wanapozipokea. Kama fedha hazijatolewa kwenye hospitali hiyo basi Wizara yangu itafuatilia ili tuweze kujua tatizo liko wapi.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya majibu!

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, labda niongezee kwenye majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri, fedha hizi za *On Call Allowance* zimeanza kutolewa toka mwezi wa pili mwaka jana na fedha zimeendelea kutolewa. Kwa bahati mbaya sana kuna baadhi ya ma- *RAS* na baadhi ya Wakurugenzi wa Halmashauri bado wamekaa na fedha hizi bila kuzitoa kwa wahusika. Tunaomba na kuchukua nafasi hii kuwaeleza kuwa fedha hizo zimekusudiwa kwa ajili ya *On Call Allowance* kwa wafanyakazi wa afya, fedha hizo zitolewe mara moja na kwa maeneo yote ambayo bado fedha hazijatolewa, tunaomba tupate taarifa ili tushughulikie mara moja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na bahati nzuri maswali pia yamekwisha.

Sasa niwatambue baadhi ya wageni walioko humu ndani, wako wageni wa Waheshimiwa Wabunge, yupo mgeni wa Mheshimiwa Ester Bulaya wakiongozwa na Ndugu Fidelis Manyerere, Mwenyekiti wa CCM Kata ya Nyaso, Musoma Mjini. Mwenyekiti Felix Manyerere naomba asimame pale alipo na hao wageni wengine wasimame pamoja. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Charles Kitwanga anaitwa Sambo Malaki Lupondije, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni nane wa Mheshimiwa Suleimani Saidi Jafo wakiongozwa na Mohammed Said Tundugulu. Wako wapi hawa? Wasimame walipo tafadhali, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wafanyakazi wawili kutoka ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ambao ni Ndugu Eribariki Lyatuu, yuko wapi na Ndugu Elieshi Saidimu, nadhani watakuja.

Tunao wageni waliokuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo, hawa ni wanafunzi sabini na Walimu kumi wa shule ya *Genius Kings Nursary* na *Primary school* kutoka Dar es Salaam. Naomba wasimame wageni wetu hao kutoka Dar es Salaam. Ahsante sana, shule inaitwa *genius* kwa hiyo na ninyi mnategemewa kuwa ma-*genius*. Karibuni sana na ahsante sana Walimu na wanafunzi wa shule hii, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna ndugu Fabiola Ndondole na Ndugu Sara Ndondole, wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge. Akina Ndondole hawa wako wapi? Ahsante sana na ninashukuru sana karibuni. *(Makofi)*

Kuna Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kusimamia na Kudhibiti Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini, Bi. Irene Isaka. Ninaomba asimame alipo, Ndugu Irene unatakiwa kukaa pale kwa Spika, mnatakiwa mumpangie pale akae, mkamhamishe pale. Ameambatana na Mwanasheria wa Mamlaka hiyo Bwana Gabo. Ahsanteni sana, ninaomba

ninyi wawili mhamie pale kwa sababu mna kazi inayoendelea hapa. *(Makofi)*

Matangazo ya Kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu ya Mashirika ya Umma, Mheshimiwa Kabwe Zitto, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa Kamati yake kuwa leo tarehe 31, saa saba na robo mchana kutakuwa na kikao cha Kamati yake katika ukumbi namba 231.

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa kujaza Fomu za Maadili umeshafika, kwa hiyo, ninawatangazieni Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Maafisa kutoka Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma wapo eneo la Bunge, sehemu ya mapokezi, kwenye jengo la Utawala kwa ajili ya kuwapatia Waheshimiwa Wabunge Fomu za kujaza mali na madeni. Wabunge wote wanaombwa kufika kuchukua fomu hizi kuanzia leo na itakapofika mwezi wa kumi na mbili ziwe zimejazwa, sitegemei mtasahau kwenda kuchukua fomu halafu mpate matatizo yaliyowahi kutokea kipindi fulani. Kwa hiyo, nendeni mkachukue fomu, mkajaze kama inavyostahili, wako pale mlangoni, ni karibu.

Tangazo linguine, Waheshimiwa Wabunge mnamwona Waziri Mkuu hayupo, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi ndiye anayeshika nafasi yake mpaka atakaporudi, ndiyo maana yuko hapo. Pia upande wa pili mnamwona Kiongozi

wa Kambi ya Upinzani hayupo, kwa niaba yake yupo Mheshimiwa Zitto ndiye anayekaimu nafasi hiyo kwa upande wa pili. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea!

KAULI ZA MAWAZIRI

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ambayo inaniwezesha kuweza kutoa Kauli ya Serikali kuhusu Fao la Kujitoa au *Withdrawal Benefit.* Lakini kabla ya kufanya hivyo na kwa idhini yako, ninaomba nitambue watu ambao wametusaidia sana katika suala hili toka Azimio la Bunge lilipotoka tulipomaliza Bunge mwezi Aprili. Ninaomba nikishukuru sana Kikosi Kazi kilichojumuisha Wizara pamoja na Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kwa kazi nzuri walioifanya na maoni waliyotuletea baada ya kuzunguka na kuonana na wadau na kutembelea nchi kadhaa za jirani ili kupata maoni yao kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Uongozi ya Bunge chini ya Uenyekiti wako na Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushauri wao tulipowapelekea suala hili. Aidha, ninapenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho kwa kuwa na ushirikiano wa karibu sana na Wizara yetu wakati

tunashughulikia suala hili. Lakini pia tunaishukuru sana Kamati ya Fedha chini ya Mheshimiwa Andrew Chenge ambaye pia ni mdau wa suala hili kwa jinsi walivyotushauri. Ninapenda pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wake katika vikao vyote vya Serikali wakati tunashughulikia suala hili kabla ya kulileta Bungeni. Pia niishukuru sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mdhibiti na Msimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa jinsi walivyolishughulikia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 49 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, ninaomba nichukue nafasi hii ili kutoa Kauli ya Serikali kuhusu marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuhusu Fao la Kujitoa na kuomba Bunge lako Tukufu kutoa muda wa Serikali wa kuwasilisha Muswada wa Marekebisho wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii unaokidhi matakwa ya Mifuko hii ambayo itakuwa ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano wa Nane katika kikao cha Bunge cha Arobaini na Moja, Bunge lako Tukufu lilipokea Hoja Binafsi iliyowasilishwa na Mheshimiwa Selemani Jafo, Mbunge wa Kisarawe ambaye miongoni mwa mambo mengine alilitaka Bunge lako Tukufu lielekeze Serikali kuandaa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii kama zilivyorekebishwa kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Na. 5 ya 2012, ili Fao la Kujitoa liweze kurejeshwa na kuwekwa kwa utaratibu wa ukokotoaji wa Fao hilo la Kujitoa kwenye Sheria; kwamba Sheria ziweke vifungu vinavyoruhusu watumishi kutumia kiasi cha mafao yao ya uzeeni kulipia

mikopo ya nyumba yaani *(home mortgage);* kwamba Sheria ziweke vifungu vinavyoruhusu watumishi kutumia kiasi cha mafao yao ya uzeeni kwa ajili ya kulipia gharama au shughuli nyingine yoyote ya kujiwekea mazingira mazuri kwa ajili ya kujiandaa na maisha ya kustaafu; na kwamba vifungu vya Sheria vinavyotamka mtumishi wa Serikali kuwasilisha maombi kwa Rais ili kupata msamaha wa kujiondoa katika Fao la Kujitoa viondolewe kwani vina urasimu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja hiyo kutolewa na kuungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge, Kiti chako kilitoa maelekezo kwa Serikali kuwa Sheria irudishwe na iangaliwe kwa utaratibu wa hali ya dharura.

Mheshimiwa Spika, hakuna ubishi kuwa hoja iliyoletwa na kuridhiwa na Bunge ilikuwa na umuhimu sana. Serikali inatambua umuhimu wa Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kwa kuzingatia uzito wa suala hili la Fao la Kujitoa, pamoja na mapendekezo yaliyojitokeza kwenye hoja ya Mheshimiwa Selemani Jafo, iliunda Kikosi Kazi ambacho kimefanya utafiti na kuandaa mapendekezo ili kuona kama kuna manufaa ya kuendelea na mfumo uliopo au kama tunahitaji mfumo mpya kama ilivyokusudiwa katika Muswada wa Sheria wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama zilivyorekebishwa katika Bunge la mwezi Aprili, 2012. Kikosi Kazi kimekamilisha taarifa yake na kuiwasilisha Serikalini.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuipitia taarifa ya Kikosi Kazi, imebaini kuwa yapo mambo ya msingi kadhaa ambayo sharti yawe yameshughulikiwa kwanza kwa kina kabla ya kuandaliwa kwa Muswada utakaokidhi matakwa

ya hoja ya Mheshimiwa Jafo kama ilivyoridhiwa na Bunge lako Tukufu Agosti 2012, ikizingatiwa kuwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ilianzishwa kwa makusudi mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali ya kiuchumi na kiutumishi hapa nchini ambayo inabidi sasa ioanishwe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, Serikali baada ya kutafakari kwa kina, imejiridhisha kuwa kurejesha Fao la Kujitoa kama ilivyokuwa katika Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2012 wakati huu, bado hatutakidhi kiu ya mabadiliko yanayohitajika ya mfumo wa sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria kuhakikisha kuwa mifuko iliyoko kwenye sekta hiyo inalinda haki za wanachama wake kwa namna inayojitosheleza.

Mheshimiwa Spika, Fao la Kujitoa kwa kawaida linatolewa kwa masharti yanayomhusu mwanachama mmoja mmoja katika mazingira pekee na mahsusi yanayomhusu mwanachama husika. Mwezi Agosti 2012, Mamlaka ya Kusimamia na Kudhibiti Mifuko ya Hifadhi za Jamii yaani *SSRA* iliagiza Mifuko iliyokuwa ikitoa Fao la Kujitoa kusitisha kufanya hivyo. Lengo kuu lilikuwa ni kuwezesha Mamlaka kutoa vikokotoo vipya vya mafao vyenye manufaa kwa wanachama bila kuathiri afya ya Mifuko husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mchakato huu ulioanza wa kuangalia upya Sheria ya Hifadhi ya Jamii, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta Hifadhi ya Jamii (SSRA) imekwishaliondoa agizo la kuzuia Mifuko kutoa Fao la Kujitoa na kufuatia hatua hiyo, Mifuko yote sasa itaendelea

kutoa fao hilo kama ilivyokuwa kabla ya zuio hilo na kwa vigezo vilevile vilivyokuwa vikitumika kwa mwanachama mmoja mmoja kadri mwanachama huyo anavyostahili kupata fao hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie sehemu hiyo:-

"Kufuatia hatua hiyo, Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii itaendelea kutoa Fao hilo la Kujitoa kama ilivyokuwa kabla ya zuio hilo na kwa vigezo vilevile vilivyokuwa vikitumika kwa mwanachama mmoja mmoja kadri anavyostahili kupata fao hilo".

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi ya kina zaidi inayohitajika kufanyika ili kuandaa Muswada utakaokidhi matakwa ya wananchi kupitia Bunge lako Tukufu, Serikali kwa kuzingatia sababu nilizokwisha kuzitaja juu na kwa ushauri wa Waheshimiwa Wadau na Wabunge wote, Serikali inaona ni busara kuondoa katika Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali sehemu inayohusu Fao la Kujitoa ili kuweza kupata muda wa kutosha kuandaa na kuleta Muswada wa Sheria utakaokidhi matakwa ya Azimio la Bunge na mahitaji ya kuwa na mfumo endelevu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inalifanyia kazi Azimio la Bunge na kabla ya kuandaa Muswada huo wa Sheria kusudiwa, Serikali itafanya majadiliano na wadau wengi zaidi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Vyama vya Wafanyakazi, Waajiri, wananchi wenyewe, sambamba na kutoa elimu kwa umma kuhusiana na suala la Fao la Kujitoa na maudhui ya Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Jafo kwa ujumla wake kama yalivyoridhiwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

MAAZIMIO

Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Pili ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jumuiya ya Nchi za Jumuiya ya Ulaya na Umoja wa Nchi za Afrika, Carribean na Pacific *(The Cotonuo Partinership Agreement).*

(Majadiliano yanaedelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, jana Azimio hili tulikuwa tumelimaliza kabisa lakini tulipofikia nafasi muhimu ya kufanya maamuzi, idadi kubwa ya Waheshimiwa Wabunge mlikuwa kwenye Kamati na kwingineko, kwa hiyo hatukuweza kufanya maamuzi lakini limejadiliwa kwa namna zote zinazostahili, sasa imebakia kuwahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Pili ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jumuiya ya Nchi za Jumuiya ya Ulaya na Umoja wa Nchi za Afrika, Carribean na Pacific (The Cotonuo Partinership Agreement) liliridhiwa na Bunge)

SPIKA: Kwa hiyo, Azimio hili limepita, likafanyiwe kazi inayostahili na kama maoni ya Wabunge wengine walivyosema kwamba hiyo Miswada inayofanyika basi ifanyike vizuri kusudi tupige maendeleo na mwisho wake nchi iweze kujitegemea yenyewe. Tunaendelea!

Azimio la Bunge la Kuridhia Kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane

na

Azimo la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mpaka na Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Gombe.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane yenye ukubwa wa kilomita za mraba 2.18 ilianzishwa kwa kupandishwa hadhi Pori la Akiba la Kisiwa cha Saanane na kujumuisha Visiwa vya Chankende Kubwa na Chankende Ndogo na eneo la maji linalozunguka visiwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Kisiwa cha Saanane lenye ukubwa...

(Hapa Katibu Mezani alikuwa akimpa maelezo Waziri)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, anachojaribu kumweleza Waziri, hapa Katibu amesoma Maazimio yote mawili kwa pamoja lakini tunakwenda moja baada ya lingine, Mheshimiwa Waziri tafadhali!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Kisiwa cha Saanane lenye ukubwa wa kilomita za mraba 0.76 linajumuisha eneo la nchi kavu na maji kwa mzunguko wa mita 100. Pori hilo lilianzishwa mwaka 1964 kwa Tangazo la Serikali Na.567 la mwaka 1964.

Lengo la kuanzishwa Pori la Akiba lilikuwa ni kuhifadhi, kulinda bioanuwai na kutoa burudani kwa wakazi wa Jiji la Mwanza na Mikoa ya jirani. Pori hilo lina mimea, wanyamapori wa aina mbalimbali waishio majini na nchi kavu pamoja na mandhari ya miamba na majabali makubwa.

Mheshimiwa Spika, visiwa vya Chankende Kubwa na Chankende Ndogo vina ukubwa wa kilomita za mraba 0.1. Visiwa hivyo vipo umbali wa wastani wa mita 500 kutoka Pori la Akiba la Kisiwa cha Saanane na vina mandhari na mimea inayofanana na ile ya Kisiwa cha Saanane. Visiwa hivyo havina makazi ya watu wala shughuli zozote halali za binadamu na vinatumika kama maficho ya wahalifu hivyo hakutakuwa na fidia yoyote.

Mheshimiwa Spika, eneo la maji lililozunguka visiwa vya Saanane na Chankende lina ukubwa wa kilomita za mraba 1.32 na ni mazalia, makazi na malisho ya samaki na viumbe wengine wa majini.

Mheshimiwa Spika, wanyamapori waliopo katika Pori la Akiba la Kisiwa cha Saanane, Visiwa vya Chankende na eneo la maji linalozunguka visiwa hivyo ni pamoja na Tumbili Weusi wa aina ya *De-brazzas* ambao wanapatikana katika visiwa hivi pekee nchini Tanzania. Wanyamapori wengine ni Fisimaji, Pakapori, Mamba, aina mbalimbali za samaki, ndege na nyoka wakiwemo Chatu.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi mahitaji ya uhifadhi endelevu wa bioanuwai na utalii ni muhimu kujumuisha Pori la Akiba la Kisiwa cha Saanane, Visiwa vya Chankende Kubwa na Chankende Ndogo na eneo la ukanda wa maji kuwa hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane. Maeneo hayo yakijumuishwa na kuwa Hifadhi ya Taifa, uhifadhi wa bioanuwai, mazalia na makuzio ya samaki na uendelezaji utalii wa Mji vitaimarika.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wanyamapori inayoelekeza kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhiwa na kulinda bioanuwai katika mtandao wa hifadhi za Taifa, Hifadhi ya eneo la Ngorongoro, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu. Vilevile kwa kuzingatia Sera ya Utalii inayolenga kukuza uchumi na maisha ya wananchi

hasa kupunguza umaskini kwa njia ya kuhimiza maendeleo ya utalii endelevu unaokubalika kiutamaduni na kijamii, unaojali mazingira na yenye faida kiuchumi, kuwepo kwa hifadhi ya Taifa katika Kisiwa cha Saanane kutachochea ukuaji wa mtandao wa utalii na uchumi wa jamii kupitia shughuli mbalimbali za utalii Kanda ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, katika kuanzisha hifadhi ya Taifa kisiwa cha Saanane, Wizara pamoja na masuala mengine imezingatia kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji uliotolewa Machi, 2006, Program ya Hifadhi ya Matumizi Endelevu ya Ziwa Victoria, Sera ya Taifa ya Uvuvi na mikakati yake ya mwaka 1997 ambayo imeweka lengo la kukuza uhifadhi na maendeleo ya usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, kukubalika kwa hoja hii kutatoa fursa za manufaa ya kimazingira, kijamii na kiuchumi kwa Taifa kama ifuatavyo:-

(i) Kuhifadhi na kuboresha ulinzi wa bioanuwai zinazopatikana ndani na pembezoni mwa hifadhi hususani mazalia, makuzio, maficho na malisho ya samaki;

(ii) Kuongezeka kwa vivutio vya utalii kutawezesha kuunda ukanda wa utalii unaojumuisha utalii wa utamaduni, fukwe, historia na wanyamapori katika Kanda ya Ziwa Victoria;

(iii) Kupanuka kwa mtandao wa utalii wa wanyamapori wa Kanda ya Ziwa Victoria na Magharibi mwa Tanzania. Ukanda huu utajumuisha hifadhi za Serengeti, Rubondo, Gombe na Mahale na Mapori ya Akiba ya Ibanda-Rumanyika, Burigi- Biharamulo-Kimisi na Moyowosi –Kigosi;

(iv) Uboreshaji wa vituo vya utamaduni na makumbusho vikiwemo Bujora, Kumbukumbu za Historia ya Biashara ya Watumwa na uvumbuzi wa chanzo cha mto Nile kwenye bandari ya zamani ya Mwanza (Mwalo wa Kageye);

(v) Kupanuka kwa wigo wa ajira kwa wananchi kupitia shughuli mbalimbali za uhifadhi na utalii;

(vi) Kuongezeka kwa fursa za uwekezaji na hivyo kukuza pato la mtu mmoja mmoja;

(vii) Kuongezeka kwa samaki na hivyo kuwanufaisha wavuvi kuvua samaki kwa uhakika pembezoni kwa hifadhi;

(viii) Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii;

(ix) Kukuza na kutangaza utajiri na utamaduni wa Mwafrika kwa kushirikiana na vituo, vikundi vya utamaduni mbalimbali; na

(x) Kuongeza utalii wa maji, utalii wa ndani, utafiti na kutoa elimu ya vitendo kwa wanafunzi na wananchi watakaotembelea hifadhi hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania, ilifanya vikao vya kuomba ridhaa katika ngazi za Kata za Butimba, Nyamagana, Igogo na Mkuyuni, Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mwanza (*RCC*). Katika vikao hivyo, hoja mbalimbali zilijitokeza na kupatiwa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

(i) Wizara kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa itaandaa mpango wa uhifadhi shirikishi wa ujirani mwema ambao wananchi watapata fursa ya kuibua miradi ya maendeleo iliyolenga kuboresha ustawi wa jamii husika;

(ii) Fursa mbalimbali za ajira zitapatikana kwa wananchi kupitia shughuli za uhifadhi na utalii;

(iii) Shughuli za uvuvi zitaendelea kufanyika pembezoni mwa hifadhi ambako kutakuwa na ongezeko la samaki kutokana na kuhifadhika kwa mazalia, malisho na makuzo;

(iv) Vyombo vya usafiri wa maji vitaendelea kupita kwenye eneo la wazi kati ya visiwa vya Chankende Kubwa na Chankende Ndogo, pia vitapita katika eneo la Ghuba ya Butimba kwa upande wa Kusini na katika Kisiwa cha Saanane na *Capripoint* kwa upande wa Kaskazini; na

(v) Tahadhari dhidi ya wanyamapori hatari hususani Mamba itachukuliwa na wananchi watahimizwa kutoa taarifa kwa Maofisa Wanyamapori ili hatua stahiki zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huo, wadau waliridhia uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane.

Mheshimiwa Spika, Wizara itashirikiana na wadau mbalimbali katika usimamizi wa hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuandaa mkakati unganishi (*integrated strategy*) ya kuongeza watalii;

(ii) Kuandaa mpango wa usimamizi na uendeshaji wa hifadhi *(General Management Plan);*

(iii) Kuweka kanuni na taratibu za usimamizi wa hifadhi na kuandaa program ya ujirani mwema;

(iv) Kuweka miundombinu inayofaa na yenye viwango vinavyokubalika ndani na nje ya hifadhi kwa ajili ya kuendeleza uhifadhi na utalii; na

(v) Kuongeza aina na idadi ya wanyama katika hifadhi kulingana na mahitaji ya kiikolojia.

Mheshimiwa Spika, mwisho ninawaomba Wabunge muunge mkono hoja ya kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Saanane yenye ukubwa wa kilomita za mraba 2.18 kwa kujumuisha Pori la Akiba la Saanane lenye ukubwa wa kilomita za mraba 0.76, Visiwa vya Chankende Kubwa na

Chankende Ndogo vyenye ukubwa wa kilomita za mraba 0.1 na eneo la maji linalozunguka Visiwa hivyo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1.32. kutokana na maelezo hayo niliyowasilisha.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nilisome Azimio lenyewe.

KWA KUWA Sera ya Wanyapori ni kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhiwa na kulinda bioanuwai katika mtandao wa Hifadhi za Taifa, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu;

NA KWA KUWA Sera ya Utalii ni kukuza uchumi na maisha ya wananchi hasa katika kupunguza umaskini kwa njia ya kuhimiza maendeleo ya utalii endelevu unaokubalika kiutamaduni na kijamii unaojali mazingira na wenye faida kiuchumi;

NA KWA KUWA Programu ya Hifadhi ya matumizi endelevu ya Ziwa Victoria, Sera ya Taifa ya Uvuvi na mikakati yake ni kukuza uhifadhi, maendeleo na usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo;

NA KWA KUWA kupandisha hadhi Pori la Akiba la Saanane pamoja na kujumuisha visiwa vya Chankande Kubwa na Chankande Ndogo na eneo la maji linalozunguka visiwa hivyo kutaimarisha uhifadhi wa bioanuwai hususani mazalia na makuzio ya samaki;

NA KWA KUWA kuanzishwa hifadhi mpya ya Taifa ya Saanane kutawezesha haja ya kuongeza spishi mbalimbali za wanyamapori na hivyo kuongeza utalii wa mjini, utalii wa ndani, utafiti na kutoa elimu ya vitendo kwa wanafunzi na wananchi watakaotembelea Hifadhi hiyo;

NA KWA KUWA Pori la Akiba la Saanane ni dogo kwa eneo hivyo kutokidhi mahitaji ya utalii pamoja na uhifadhi endelevu wa bioanuwai;

NA KWA KUWA Visiwa vya Chankende Kubwa na Chankende Ndogo na Pori la Akiba la Saanane ni makazi pekee nchini ya Tumbili Weusi aina ya *De-brazzas* na pia eneo la ukanda wa maji wa mita 100 unaozunguka visiwa hivyo ni mazalia na makuzio ya samaki;

NA KWA KUWA Visiwa vya Chankende Kubwa na Chankende Ndogo havina makazi ya watu na vinatumika kama maficho ya wahalifu;

NA KWA KUWA Pori la Akiba la Saanane, Visiwa vya Chankende Kubwa na Chankende Ndogo na eneo la ukanda wa maji yakijumuishwa na kupandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa, hali ya uhifadhi wa bioanuwai, uhifadhi wa mazalia na makuzio ya samaki na uendelezaji utalii wa mjini vitaimarika;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura ya 282 kama ilivyorekebishwa mwaka 2002, ili kuanzisha Hifadhi ya Taifa ni

sharti kupata ridhaa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

HIVYO BASI Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkutano wake wa Tisa sasa linaridhia, Hifadhi ya Taifa ya Saanane yenye ukubwa wa kilomita za mraba 2.18 ianzishwe kwa kujumuisha Pori la Akiba la Saanane lenye ukubwa wa kilomita za mraba 0.76, Visiwa vya Chankende Kubwa na Chankende Ndogo vyenye ukubwa wa kilomita za mraba 0.1 na eneo la maji linalozunguka Visiwa hivyo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1.32.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja iimeungwa mkono, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia hoja hii au mwakilishi wake, Mheshimiwa Amina Clement.

MHE. AMINA A. CLEMENT (K.n.y. MHE. JAMES D. LEMBELI-MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILINA MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane kama ilivyoanishwa na Kanuni 114 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu haikupata muda wa kutosha kutafakari na kujadili Hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane. Jana, Jumanne tarehe 30 Oktoba 2012, Kamati ilikutana na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Balozi Khamis S. Kagasheki ili kupata maelezo na ufanunuzi kuhusu kupandisha hadhi Pori la Akiba la Saanane pamoja na kujumuisha Visiwa vya Chankende Kubwa na Chankende Ndogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba Pori la Akiba la Kisiwa cha Saanane lilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Namba 567 la mwaka 1964 kwa lengo la kuhifadhi, kulinda bioanuwai na kutoa burudani kwa wakazi wa Jiji la Mwanza na Mikoa ya jirani. Kwa muda mrefu sasa tangu kuanzishwa kwa Pori la Akiba la Kisiwa cha Saanane kumekuwa na mafanikio yasiyokidhi malengo yaliyokusudiwa kuanzishwa kwa Pori hilo, kwa mfano eneo la Pori la Akiba kuwa dogo na hivyo kutokidhi mahitaji ya utalii pamoja na uhifadhi endelevu wa bioanuwai.

Aidha, Visiwa vya Chakende Kubwa na Chakende Ndogo ambavyo vinazunguka Pori la Akiba la Kisiwa cha Saanane hakuna makazi ya watu wala shughuli halali za binadamu na mara nyingi visiwa hivyo hutumika kama maficho ya wahalifu. Vilevile, Kamati ilielezwa kuwa hatua zote za ushirikishwaji wa wananchi zilifuatwa na kuridhiwa katika ngazi ya Kata, Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mwanza (*RCC*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imejitathimini yenyewe na kutambua kwamba ikiwa Pori la Akiba la Kisiwa vya Saanane na Visiwa vya Chakende Kubwa na Chakende Ndogo vikipandishwa hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa itaweza kuendeleza maeneo hayo kwa lengo la kudumisha uhifadhi endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo na kuimarisha uhifadhi wa bioanuwai hususani mazalia ya samaki. Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa uamuzi huo na inakubaliana na Azimio hili la kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane, Kamati imeridhika na sababu zilizowasilishwa na Waziri wa Maliasili na Utalii na kuona ni za msingi na zenye manufaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwatambua kwa majina wajumbe wa Kamati hii Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdulkarim E. Hassan. Shah, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mheshimiwa Philemon K. Ndesamburo, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Ali khamis Seif, Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Bernadetha K. Mushashu, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Michael Lekule laizer, Mheshimiwa Kaika Saning‘o Telele, Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa,

Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa, Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali na Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii pia kumshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Balozi Khamis S. Kagasheki na Wataalam wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ufafanuzi mzuri walioutoa wakati Kamati ilipokuwa ikichambua Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuwezesha Kamati kukamilisha kazi hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu. Grace Bidya na Ndugu Rachel Nyega kwa kuratibu shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio hili, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa ingawa Mchungaji mwenzenu amesema nisiwaite hivyo, Mchungaji mwenzenu juzi amesema nisiwaite hivyo lakini nitawaita hivyo, Mchungaji Msigwa.

MHE. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kabla ya yote, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru Madaktari wa *MOI* kwa kunitibu mguu wangu vizuri na ninaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika kulifanya Bunge liweze kuazimia Azimio hili, ni vema Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, ikaliambia na kulihakikishia Bunge juu ya uzingatiaji wa Sheria ya Ardhi katika ubadilishaji wa matumizi ya ardhi ikizingatiwa ardhi yote katika nchi hii ina matumizi ambayo yapo bayana kwa kile kinachofanyika katika ardhi husika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kutokana na Azimio hili kutaka Bunge liweze kuridhia uanzishwaji wa hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane na kwa kuwa Azimio linataka kuongeza ukubwa wa hifadhi na kuongeza Visiwa vya Chankende Kubwa na Ndogo, ni vyema Serikali ikaweka uzingatiaji wa sheria na mchakato wa kisheria katika kulifanikisha hilo ili kutoweza kuingia katika migogoro ya ardhi kama ilivyo katika maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mwanza ni moja ya Mikoa michache hapa nchini iliyo na vivutio vingi vya utalii vinavyoweza kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa ambavyo Serikali bado haijavitangaza kiasi cha kutosha. Kuna nchi zenye vivutio vichache duniani kama Botswana na Mauritius lakini nchi hizi zimefaulu kujiletea mapato makubwa. Kwa hiyo, Serikali ikiviboresha na kuvitangaza

vinaweza kuingiza mapato makubwa kwa ajili ya kujiletea maendeleo katika Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na lengo la Serikali la kuleta Azimio hili na Bunge kuridhia, pia Serikali ihakiki na kurejea upungufu uliomo katika kukuza sekta ya utalii ikiwa ni pamoja na kutotangaza vivutio kama hivi, pamoja na kuzingatia shabaha ya kuanzishwa kwa hifadhi ikiwa ni kuhamasisha uhifadhi na kuelimisha jamii juu ya utalii pamoja na kutoa fursa kwa wakazi wanaozunguka hifadhi katika uendelezaji na utalii ikiwa ni pamoja na kushiriki kutalii, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali pamoja kufanya juhudi za kuanzisha hifadhi na kupandisha hadhi baadhi ya hifadhi ambalo ni jambo jema kwa Serikali na jamii pia, izingatie suala la kuzitangaza vema ili ziweze kuwa na tija katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Naona hili jambo liko wazi kabisa, kwa hiyo, mtoa hoja, hakuna walioomba kuchangia.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuzungumzia yafuatayo kuhusu masuala ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani imeyazungumza hapa. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba masuala ya ardhi, hapa tulizungumza na Wizara ya Ardhi ilikuwemo katika mchakato huu, ngazi ya Taifa na pia ngazi ya Mkoa wa Mwanza. Lakini jambo la pili ni lile nililosema

katika hoja yangu kwamba Kisiwa cha Saanane tangu awali mwaka 1964 kilikuwa ni kisiwa ambacho kilikuwa kina wanyama na watu walikuwa wanakwenda pale kutembea. Vile Visiwa viwili vya Chankende ambavyo vilikuwa ni mapendekezo yaliyotoka kwa wananchi husika wenyewe ni kwa sababu ilikuwa ni fichio la majambazi na wezi na kulikuwa hakuna watu mpaka leo ambao wanaishi katika maeneo hayo. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba hayo yote tuliyazingatia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jambo la pili ambalo amelizungumzia Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu kutangaza maeneo haya ya kitalii ambayo tulikuwa nayo ni kwamba ni jambo ambalo tunalifanya na mawazo ambayo ameyatoa nataka nimhakikishie kwamba tutayazingatia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa shukrani zangu kwamba pendekezo letu la kuweza kupandisha Kisiwa cha Saanane kikawa Hifadhi na kama itakuwa imepita itakuwa ni Hifadhi ya 16 maana tunazo 15, hii itakuwa ni ya 16. Kwa hiyo, naomba kwa niaba ya Wizara yangu kutoa shukrani zetu kwa Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Bunge la Kuridhia Kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane liliridhiwa na Bunge)

SPIKA: Tunaendelea, Katibu!

Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mpaka na Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Gombe.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa Gombe ilianzishwa mwaka 1968 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 33.74. Lengo la kuanzishwa kwake ni kuhifadhi na kutoa ulinzi madhubuti kwa bioanuai hususani wanyamapori aina ya Sokwemtu ambao ni adimu Duniani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Sokwemtu, Hifadhi hii ina vivutio vya chemichemi, maporomoko ya maji ya mito ya Kakombe na Mkenke ambayo hutiririka na kuingia Ziwa Tanganyika. Vilevile kuna misitu, milima na mabonde yanayohifadhi wanyamapori wengine wakiwemo aina ya Nyani wa Kijivu, Mbega Mwekundu, Kima mwenye mkia wa bluu na mwekundu na kima chotara. Wengine ni Pongo, Ndege wa aina mbalimbali na nyoka wakiwemo chatu. Bioanuai hizi zimeifanya Hifadhi ya Taifa ya Gombe kuwa moja ya vivutio vya utalii katika bonde la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ilipoanzishwa mwaka 1968 iliacha nje ufukwe wa Ziwa Tanganyika kwa upana wa mita 90 zinazoambaa na mpaka wa Magharibi mwa Hifadhi kwa urefu wa kilomita 14. Ufukwe huo ulitumiwa na wavuvi kukokora samaki, kuanika dagaa na kuweka makambi. Kutokana na mwingiliano wa shughuli za uvuvi na uhifadhi,

Nyani huwanyang'anya wavuvi dagaa na Sokwemtu kunyang'anya chakula cha wavuvi pamoja na uvuvi wa makokoro kuonekana siyo endelevu, mwaka 1998 Serikali ilipiga marufuku uvuvi huo. Kufuatia uamuzi huo wa Serikali, eneo la ufukwe limekuwa halitumiki tena hivyo kurudi katika hali yake ya asili.

Mheshimiwa Spika, eneo la Hifadhi ya Taifa Gombe halikidhi mahitaji ya kuwa na mfumo timilifu wa kiikolojia. Hali hii inatokana na mpaka wa hifadhi kuacha nje eneo la ufukwe na ukanda wa maji wa Ziwa Tanganyika ambalo ni muhimu kwa maisha ya Sokwemtu, mazalia, maficho, malisho na makuzio ya samaki na viumbe wengine wa majini.

Mheshimiwa Spika, ufukwe ulio nje ya mipaka ya hifadhi umekuwa ukitumiwa na Sokwemtu kubarizi hivyo kufanya waonekane kwa watalii bila kulipa ada au kuingia hifadhini. Hali hii inasababisha Serikali kupoteza mapato ya wastani wa dola za kimarekani mia moja kwa siku kwa kila mgeni wa nje. Vilevile kwa kuchangia matumizi ya ufukwe kati ya binadamu na Sokwemtu kumekuwepo na hatari ya maambukizi ya magonjwa baina yao.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na taasisi ya Jane Goodall iliyopo hifadhini ilihusisha na utafiti wa Sokwemtu na wanyama jamii ya Nyani tangu mwaka 1960, umebaini kuwa magonjwa ya kuambukizana ni mafua, homa ya mapafu, uti wa mgongo, kifua kikuu na upele. Takwimu

zilizopo zinaonesha asilimia 60 ya vifo vya Sokwemtu vinatokana na maambukizi ya magonjwa hayo.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa Hifadhi, kumekuwepo na changamoto ya mpaka kati ya hifadhi na vijiji vya Mtanga na Mwamgongo. Kwa upande wa Kusini, asilimia 80 ya eneo la makaburi ya kijiji cha Mtanga katika kitongoji cha Kazinga yapo ndani ya Hifadhi. Vilevile kwa upande wa Kaskazini, nyumba saba na baadhi ya mashamba ya wananchi wa Kijiji cha Mwangongo yapo ndani ya Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, katika kutafuta suluhu ya changamoto ya mipaka ya hifadhi na Vijiji vya Mtanga na Mwamgongo, Wizara ilifanya vikao na wanavijiji wa Mtanga na Mwamgongo, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Mkoa wa Kigoma. Katika vikao hivyo tulikubaliana kama ifuatavyo:-

(i) Eneo la kilomita za mraba 0.2 linalojumuisha makaburi, mashamba na nyumba saba liachwe nje ya mipaka ya Hifadhi;

(ii) Eneo la ufukwe lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1.26 lijumuishwe kwenye Hifadhi ya Taifa ya Gombe;

(iii) Ukanda wa maji wenye ukubwa wa kilomita za mraba 21 ujumuishwe kwenye Hifadhi ya Taifa Gombe; na

(iv) Hakutakuwa na fidia yoyote itakayotokana na maamuzi hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi mahitaji ya uhifadhi endelevu na bioanuai na utalii, ni muhimu kujumuisha eneo la ufukwe na ukanda wa maji kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa Gombe. Maeneo hayo yakijumuishwa yatafanya Hifadhi ya Taifa Gombe kuwa na ikolojia timilifu hivyo kuboresha uhifadhi wa bioanuai, mazalia, makuzio ya samaki na viumbe wengine wa majini.

Halikadhalika, kuongezeka kwa ukubwa wa Hifadhi ya Taifa Gombe na ukaribu wake na Hifadhi ya Taifa ya Mahale, Katavi na Mapori ya Akiba ya Ugalla, Kigosi na Moyowosi kutaboresha shughuli za vivutio vya utalii katika ukanda wa utalii wa Magharibi mwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wanyamapori inayoelekeza kudumisha uhifadhi endelevu na kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhiwa na kulinda bioanuai katika mtandao wa Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu.

Vilevile kuzingatia Sera ya Utalii iliyolenga kukuza uchumi na maisha ya wananchi hasa katika kupunguza umaskini kwa njia ya kuhimiza maendeleo ya utalii endelevu unaokubalika kiutamaduni na kijamii, unaojali mazingira na wenye faida kiuchumi, marekebisho ya mpaka wa Hifadhi

ya Taifa Gombe yataboresha mahusiano na ukuaji wa mtandao wa utalii na uchumi wa jamii kupitia shughuli mbalimbali za utalii.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza Hifadhi ya Taifa Gombe, Wizara pamoja na masuala mengine imezingatia kutekeleza mkakati wa Taifa wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji uliotolewa Machi 2006; Programu ya Hifadhi ya Matumizi Endelevu ya Bonde la Ziwa Tanganyika; Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati yake ya mwaka 1997 ambayo imeweka lengo la kukuza uhifadhi, maendeleo na usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, kukubalika kwa hoja hii kutatoa fursa za manufaa ya kimazingira, kijamii na kiuchumi kama ifuatavyo:-

(i) Kuimarisha uhifadhi na ulinzi wa Wanyamapori waliohatarini kutoweka hususani Sokwemtu;

(ii) Kuboresha uhifadhi madhubuti wa Bioanuai yakiwemo mazalia, makuzio, makazi, maficho na malisho ya samaki na viumbe wengine wa majini;

(iii) Utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kimataifa ya uhifadhi wa mazingira na viumbe walio hatarini kutoweka ambao Tanzania imeridhia;

(iv) Kuongezeka kwa shughuli za utalii kama vile kuogelea, utalii wa mitumbwi na uvuvi wa burudani ambao jamii inayozunguka Hifadhi itapata fursa ya kushiriki na kunufaika;

(v) Mapato yaliyokuwa yanapotea kutokana na watalii waliokuwa wanawaona Sokwemtu bure ufukweni yatadhibitiwa hivyo kuongeza kipato cha Hifadhi na uchangiaji wa miradi ya maendeleo kwa jamii inayozunguka Hifadhi;

(vi) Kutatua migogoro iliyokuwepo kati ya Hifadhi na vijiji vya Mtanga na Mwamgongo na hatimaye kuimarika kwa mahusiano ya Hifadhi na Jamii inayozunguka;

(vii) Kupanuka kwa wigo wa ajira kwa wananchi hasa kwenye shughuli zinazoendana na utalii;

(viii) Kuongezeka kwa uhakika wa upatikanaji wa samaki kwa jamii kutokana na uvuvi pembezoni mwa Hifadhi;

(ix) Vyombo vya usafiri wa abiria vitaendelea kupita kwa usalama kwenye eneo la maji ya Hifadhi; na

(x) Ari ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya ujirani mwema kwa vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Gombe itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, Wizara itashirikiana na wadau katika usimamizi wa Hifadhi ya Taifa Gombe kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuandaa mkakati unganishi *(integrated strategy)* ya kuongeza utalii;

(ii) Kupitia mpango wa usimamizi na uendeshaji wa Hifadhi hii kujumuisha eneo la ufukwe wa ukanda wa maji;

(iii) Kuendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya eneo la ufukwe na ukanda wa maji hususani kuruhusu vyombo vya usafiri wa maji kupita ndani ya eneo la Hifadhi pamoja na matumizi ya maji; na

(iv) Kuweka miundombinu inayofaa na yenye viwango vinavyokubalika ndani na nje ya Hifadhi kwa ajili ya kuendeleza utalii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumaliza kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge muunge mkono hoja hii ya marekebisho ya mpaka na upanuzi wa Hifadhi ya Taifa Gombe kutoka kilomita za mraba 33.74 na kuwa kilometa za mraba 56 kutokana na manufaa niliyoyaeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Sawa nakubali. Mheshimiwa Waziri hujamaliza, Azimio lenyewe halijasomwa.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nisome Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

KWA KUWA, Sera ya wanyamapori ni kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhiwa na kulindwa bionuwai katika mtandao wa Hifadhi za Taifa, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu;

NA KWA KUWA, ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya ardhi za Vijiji na maeneo yaliyohifadhiwa inapatiwa ufumbuzi wa kudumu;

NA KWA KUWA, Tanzania imeridhia mikataba ya Kimataifa ya kuhifadhi wanyama adimu na walio hatarini kutoweka hususan Sokwemtu ambao pia wanapatikana katika Hifadhi ya Taifa Gombe;

NA KWA KUWA, eneo la hifadhi ya Taifa Gombe kwa sasa halikidhi mahitaji ya kuwa na mfumo timilifu wa kiikolojia kwa kuacha nje eneo la ufukwe na ukanda wa maji wa Ziwa Tanganyika ambalo ni muhimu kwa uhifadhi wa mazalia, maficho, malisho na makuzio ya samaki na viumbe wengine wa majini;

NA KWA KUWA, Sokwemtu wanaopatikana katika Hifadhi ya Gombe wanapenda kubarizi katika ufukwe ulio nje ya hifadhi, hivyo kufanya waonekane kwa watalii bila kulipa ada ya kuingia Hifadhini;

NA KWA KUWA, kumekuwepo na muingiliano wa magonjwa kama vile mafua na upele baina ya Binadamu

na Sokwemtu unaosababishwa na kuchangia eneo la ufukwe;

NA KWA KUWA, kuwa kujumuisha eneo la ufukwe za Ziwa na ukanda wa maji ulioko nje ya mipaka ya hifadhi kutawezesha Hifadhi ya Taifa Gombe kuwa na mfumo timilifu wa kiikolijia;

NA KWA KUWA, kuongezeka kwa eneo la ufukwe na ukanda wa maji kwenye eneo la Hifadhi kutaongeza wigo wa shughuli za utalii katika Hifadhi kama vile kuogelea, utalii wa boti na mitumbwi, na uvuvi wa kitalii;

NA KWA KUWA, kuongezeka kwa ukubwa wa Hifadhi ya Gombe na ukaribu wake na Hifadhi ya Gombe na ukaribu wake na Hifadhi za Taifa za Mahale, Katavi na Mapori ya Akiba ya Ugalla, Kigoyowosi kutaboresha shughuli na vivutio vya utalii katika ukanda wa utalii wa Magharibi mwa Tanzania;

NA KWA KUWA, kuna haja ya kuweka bayana mipaka kati ya hifadhi ya Taifa Gombe na vijiji vya Mwamgongo na Mtanga kwa kuondoa eneo la mashamba na nyumba sana zilizoko kaskazini mwa Hifadhi na eneo la makaburi lililopo kusini mwa Hifadhi;

NA KWA KUWA, ili kuwezesha mabadiliko ya mipaka ya hifadhi ya Taifa Gombe kwa kuondoa eneo la mashamba,

nyumba sana na makaburi na kujumuisha eneo la ufukwe na ukanda wa maji wa Ziwa Tanganyika kuwa sehemu ya hifadhi ya Taifa Gombe, ridhaa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inahitajika;

HIVYO BASI, kwa mujibu wa kifungu cha tatu na cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkutano wake huu wa Tisa linaomba kuridhia marekebisho ya mipaka ya Hifadhi ya Taifa Gombe kutoka kilomita za mraba 33.74 na kuwa kilomita za mraba 56 kwa kuondoa eneo la makaburi, mashamba na nyumba saba lenye ukubwa wa kilomita za mraba 0.2 na kujumuisha eneo la ufukwe la Ziwa Tanganyika lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1.26 na eneo la ukanda wa maji lenye ukubwa wa kilomita za mraba 21 kwa upande wa Magharibi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti au Mwakilishi wa Kamati iliyoshughulikia Azimio hili. Mheshimiwa Lembeli.

MHE. JAMES D. LEMBELI - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, awali ya

yote nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mpaka na Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Gombe, kama ilivyoanishwa na Kanuni ya 114 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 30 Oktoba, 2012 Kamati yangu ilikutana na Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki - Waziri wa Maliasili na Utalii na baadhi ya Watendaji kutoka Shirika la Hifadhi la Taifa Tanzania *(TANAPA)* na kupata fursa ya kutafakari na kujadili Hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia marekebisho ya mpaka na upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Gombe. Kamati ilipokea maelezo na ufafanuzi kuhusu umuhimu wa upanuzi wa Hifadhi hii na Kuridhia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Hifadhi ya Taifa ya Gombe ina Sokwemtu wa kipekee ambao hawapatikani popote ulimwenguni, hivyo kuongeza umuhimu wa kuwa na mfumo timilifu wa kiikolojia wa kuhakikisha wanyama hawa wanahifadhiwa vizuri ili wasitoweke, bado kuna faida nyingi zitakazopatikana kimazingira, kijamii na kiuchumi endapo marekebisho ya mpaka yatafanyika na hifadhi kupanuliwa. Faida hizo ni pamoja na:-

(i) Kuboresha uhifadhi madhubuti wa bioanuwai yakiwemo mazalia ya samaki, makuzio, makazi, maficho na malisho ya samaki na viumbe wengine wa majini;

(ii) Kutatua migogoro iliyokuwepo kati ya Hifadhi na Vijiji vya Mtanga na Mwamgongo ambapo ardhi ya Vijiji hivi itarejeshwa kutoka katika eneo la Hifadhi na hivyo kuimarisha mahusiano ya Hifadhi na Jamii inayozunguka;

(iii) Kuongezeka kwa shughuli za utalii kama vile kuogelea, utalii wa mitumbwi na uvuvi wa burudani, ambapo jamii inayozunguka hifadhi itapata fursa ya kushiriki;
(iv) Kutakuwa na ongezeko la mapato yanayotokana na utalii, kwani mapato yaliyokuwa yanapotea kwa watalii kuona Sokwe walioko katika fukwe bure yatadhibitiwa na hivyo mapato hayo kuwezesha uchangiaji wa miradi ya maendeleo kwa jamii inayozunguka Hifadhi hiyo;

(v) Kukuza uchumi wa wananchi wanaotegemea uvuvi, kwani samaki wanategemea kuongezeka kutokana na eneo la mazalia kulindwa kama ilivyo katika Hifadhi jirani ya Mahale; na

(vi) Kupanua wigo wa ajira kwa wananchi hasa kwenye shughuli zinazoendana na utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Kamati yangu imeona kwamba, endapo Bunge lako Tukufu litaridhia Azimio hili, faida zitakazopatikana kwa Jamii inayozunguka Hifadhi hii na Taifa kwa ujumla ni nyingi. Hivyo basi, Kamati imeridhika na sababu za kurekebisha mpaka wa hifadhi hii kama zilivyoelezwa na Waziri mwenye dhamana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kumega eneo la Hifadhi na kulitoa kwa wananchi.

Hatua hii ni ya kiungwana na ni ya kupongezwa, kwani itaongeza imani ya wananchi kwa Serikali.

Aidha, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kuwasilisha Azimio lenye lengo la kuifanya Hifadhi ya Taifa ya Gombe kuwa na ikolojia timilifu, hivyo kuboresha uhifadhi wa bioanuwai na mazalia na makuzio ya Samaki. Hata hivyo, pamoja na nia hii njema ya Serikali ambayo Kamati imeunga mkono, bado kuna baadhi ya maeneo ambayo Kamati inatoa angalizo na kuishauri Serikali ifuatavyo:-

(i) Elimu kuhusu umuhimu wa kutunza na kuhifadhi eneo la Hifadhi hii na hasa eneo la ziwa linaloongezwa iendelee kutolewa kwa jamii ili wananchi wa eneo hili wahamasike kulinda mazalia ya samaki na hatimaye kuwa na uvuvi endelevu;

(ii) Ili kuondoa migogoro yoyote inayoweza kutokea baina ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa na wananchi wanaojishughulisha na uvuvi, ni vyema basi kukawekwa alama ya mpaka wa Hifadhi katika eneo la Ziwa mara tu mpaka rasmi utakapojulikana; na

(iii) Kwa kuwa eneo lililokuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Gombe kuanzia mwaka 1968, sasa linatarajia kurudishwa kwa Vijiji vya Mwamgongo na Mtanga, Serikali iweke mikakati madhubuti ya kuwaelimisha wananchi wa maeneo hayo umuhimu wa kuendelea kuyatunza mazingira hayo ambayo pia yana misitu na uoto wa asili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, sasa naomba kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa James Daudi Lembeli - Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdulkarim E. Hassan Shah - Makamu Mwenyekiti, na Wajumbe ni Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Christopher Olesendeka, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Ali khamis Seif, Mheshimiwa Suzan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Bernadetha K. Mushashu, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Michael Lekule laizer, Mheshimiwa Kaika Saning‘o Telele, Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa na Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng‘ong‘o. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, na Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Balozi Khamis J. S. Kagasheki -

Waziri wa Maliasili na Utalii na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano alioipa Kamati ilipokuwa ikifikiria Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote imefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, Makatibu wa Kamati - Ndugu Rachel Nyega na Grace Bidya kwa kuratibu shughuli zote za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani na dhana nzima ya upanuzi wa mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Gombe, japokuwa kuna mambo kadhaa ambayo tunaona inabidi yapatiwe ufumbuzi kabla ya utekelezaji huo wa upanuzi kuanza rasmi.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa, kabla ya uanzishwaji rasmi wa Hifadhi hiyo ya Gombe hapo mwaka 1968, eneo hilo lilimilikiwa na wananchi ambao baadhi yao mpaka wakati huu ninaposoma hotuba hii bado wapo na wanaendelea kuidai Serikali, kwani walikuwa wanamiliki

mashamba ya michikichi. Kilio cha wakazi wa Mwamgongo kuhusu malipo ya fidia kwa uanzishwaji wa Hifadhi ya Gombe mwaka 1968 ni madai halali kabisa na yanapaswa kuzingatiwa na Serikali kwa kuwapa kifuta machozi.

Hivyo basi, itakuwa ni busara kwa Serikali kuwalipa wazee hao ili nao wajione kuwa ni sehemu muhimu katika Hifadhi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aya ya sita ya Azimio inasema kuwa, moja ya sababu za kutaka eneo la ufukwe wa Ziwa Tanganyika kuwa sehemu ya Hifadhi ni kuepusha magojwa ambayo yanaambukizwa kutoka kwa wanyama, yaani Sokwemtu. Kwani mara nyingi Sokwemtu wanapenda kubarizi eneo hilo la ufukwe. Aidha, katika aya ya nane inajikita kueleza faida za kuongezeka wigo wa shughuli za kitalii katika ufukwe huo kama vile, kuogelea, utalii wa boti na mitumbwi na uvuvi wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa sababu iliyotolewa katika aya ya sita inajichanganya na ile ya aya ya nane, kwani kama kweli tuko makini inaweza kusababisha watalii wakakoma kabisa kutembelea Hifadhi hiyo kutokana na magonjwa kama itatokea yakawakumba watalii. Hii inaashiria hatari inayoweza kujitokeza hapo baadaye kwani kinyume cha matarajio ya upanuzi kinaweza kuwa ni kilio kwa uchumi wa nchi na wananchi wa Kigoma kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Hifadhi kuachia baadhi ya maeneo yaliyokuwa ndani ya mipaka yake hali yakitumiwa na Wanavijiji wa Mwamgongo na Mtanga, ni jambo ambalo linakaribisha mahusiano mema kati ya

Hifadhi na jamii zinazozunguka hifadhi. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitizi kuwa migogoro inayoendelea hivi sasa baina ya jamii na maeneo mengine ya Hifadhi katika nchi hii hayatakiwi kuwepo kama busara zitatumika zaidi kama ilivyotokea katika hili kuliko nguvu.

Vile vile tunapendekeza kwamba miradi ya ujirani mwema sasa hivi iwe ni miradi ya kuongeza kipato cha wananchi.

Mfano, hivi sasa Serikali ya Kijiji cha Mwamgongo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ufundi cha Berlin Ujerumani, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mbunge wa Jimbo husika yaani Mheshimiwa Zitto, wameanzisha mradi wa '*eco-tourism'* ambao utakifanya Kijiji cha Mwamgongo kuwa Kijiji cha kwanza Tanzania kuwa na umeme kila nyumba, kufungua nyumba za wageni na ukumbi wa wageni na kuweka mfumo wa maji safi na majitaka kwa kutumia umeme wa jua.

Hata hivyo mradi haujapata msaada wowote wa Shirika la *TANAPA* licha ya juhudi za Halmashauri ya Wilaya Kigoma. Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba Miradi ya *TANAPA* kwenye maeneo ya Vijiji vinavyopakana na Hifadhi iwe ya kuzalisha mapato, kukuza uchumi na kupunguza umasikini kwa kupitia utalii *(Community Based Tourism)*. *TANAPA* pia isaidie wakazi wa Vijiji vya Mwamgongo na Mtanga kufanya uvuvi wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, ukanda wa maji wenye ukubwa wa kilometa za mraba 21 ambao unajumuishwa katika eneo la hifadhi, ni faida kubwa sana, kwani kumekuwepo kwa

matukio mengi yanayohusu uharamia unaohusisha wavuvi kuporwa samaki na vitendea kazi vyao. Hivyo basi, hatua ya eneo hili kuwa muda wote chini ya uangalizi wa Askari wa Hifadhi, ni hatua muhimu ya kukabiliana na janga hilo, na hii ni mojawapo ya faida za upanuzi wa mipaka ya hifadhi.

Hata hivyo, matukio ya ujambazi dhidi ya wavuvi katika Ziwa Tanganyika yanapaswa kutazamwa kwa ukaribu na Serikali maana sasa imekuwa ni kazi ya wavuvi kuchanga fedha kwa ajili ya kulipia wanajeshi wanaokwenda kuwalinda wanapovua. Hii siyo sawa, maana wananchi wanalipa kodi ili Serikali iwalinde. Kwanini Serikali inakwepa jukumu lake la kulinda Raia wake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa naomba kutoa pongezi na shukrani nyingi kwa wanachama, wapenzi na wengine wote ambao kwa moyo mmoja walishirikiana na viongozi wetu kuhakikisha tunafanya vizuri katika chaguzi za Udiwani zilizomalizika hivi karibuni. Namshukuru sana Mungu kwa kuninusuru kwenye mikono ya vibaka walionishambulia mimi na dereva wangu *Ocean Road* karibu na Ikulu, tarehe 25 Oktoba, 2012. Shambulio hilo lilinipa maumivu makali ikizingatiwa kuwa ningali bado nauguza mguu. Jambo hili linaashiria kuwa usalama wa raia nchi hii uko tete. *(Makofi)*

Sambamba na hilo, ni shukrani kwa wananchi wa Jimbo langu la Iringa Mjini kuendelea kuniunga mkono katika kipindi hiki kigumu ambacho ninauguza mguu wangu na hivyo kushindwa kufika katika maeneo ya Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa uendelee na kuwasilisha yale ya kwako pia. Kaendelee kuwasilisha na ya kwako, si umeomba kuchangia pia? Kachangie sasa! Ameomba Kambi Rasmi ndiyo amemaliza sasa. Pia akaomba kuchangia, sasa namteua akachangie kwanza. Wewe uchangie sasa, tusikilize tofauti inakuaje. *(Kicheko)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa juhudi kubwa ambazo wamezifanya katika kupanua hii mipaka. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Kagasheki, mimi kama Waziri Kivuli nikifanya kazi yangu, *it is not personal*, najitahidi kufanya kazi yangu kama Waziri Kivuli kuhakikisha tunakuwa na uhifadhi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikubwa kama nilivyosema, napongeza sana. Mimi nina jambo moja tu pamoja na uhifadhi na mipaka tunayoongeza, lakini jambo moja ambalo nilitaka kuzungumza, Hifadhi hizi ambazo tulizonazo, pamoja na kwamba tunaongeza mipaka ambalo ni jambo zuri, Baba wa Taifa huko nyuma, na ukiangalia hata Wakoloni waliokuwepo, waliona rasilimali tulizonazo. Kwa hiyo, walizilinda, waliziwekea mipaka.

Mheshimiwa Spika, ninaamini, mimi kama Mchungaji na kama mnavyoniita, Biblia yangu hii inasema, utukufu wa nyumba ya mwisho unakuwaga ni mzuri kuliko wa nyumba iliyopita. Naamini sisi wa sasa tuna uelewa mzuri, tuna vitendea kazi vizuri kuliko Wakoloni, kwa hiyo, tuna wajibu wa kuhakikisha hizi rasilimali ambazo Mungu alitupa tunazihifadhi vizuri. Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipaka hii tunayoipanua, tunaihifadhi, lakini hivi karibuni kumekuwa na matukio ambayo yanasikitisha kuonyesha kwamba uhifadhi huu hauendani kabisa na jinsi ambavyo tunataka tufanye. Matukio ya meno ya tembo kupatikana huko China, inaonyesha jinsi gani ambavyo tembo wetu wanauliwa.

Matukio ya juzi ambayo tumeona meno ya tembo yamekamatwa Dar es Salaam, inaonyesha ni jinsi gani ambavyo tembo wanateketea. Kwa hiyo, naomba Serikali ichukue hatua za makusudi pamoja na mipango mizuri ya Wizara ya kuhakikisha kwamba tunaweka mipaka mizuri, tusigombane na raia wetu, lakini uhifadhi na ulinzi wa maliasili yetu ni wa muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Waziri Kivuli sifurahishwi sana na kusikia meno ya tembo yamekamatwa, kwa sababu hii inaashiria kwamba tembo wamekufa tayari. Kwa mfano, ukihesabu meno ya tembo 104 maana yake wamekufa tembo, au ndovu 50. Ukienda ile ya China ni kama tembo elfu moja kitu wamekufa. Kwa hiyo, kukamatwa haitusaidii, kuliko kuzuia hao tembo wasife. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwamba tufanye juhudi za makusudi, tumekwenda kwenye mapori mengine watu wamevamia

nchi, ni kama vile hii nchi haina mwenyewe, ili tulinde maliasili kwa ajili ya vizazi vinavyokuja.

Mheshimiwa Spika, kuwa kwenye *front pages* za magazeti haziwezi kupunguza uhalifu, ni lazima tuwe *strategically*, tupange mikakati mizuri ambayo itasababisha wanyama wetu walindwe. Hili ni janga la Kitaifa kwa sababu kwa kweli wanyama wanapotea. Ningeiomba niisihi Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo langu ni hilo kubwa ambalo ningeiomba Serikali inayojiita ni sikivu, hili suala siyo la mchezo, wanyama wanateketea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Kwani Kambi ya Upinzani walikataa hayo mpaka yakawa ya kwako hayo, na yale mengine ya Kambi ya Upinzani? Ahsante kwa maoni. Yaani nasema hayo ungesema kwenye hotuba yako, ingekuaje? Hayo uliyoyasema sasa hivi, ungeandika mle yangekuaje? Yangekuwa mabaya hayo? Mbona yalikuwa mema tu? Ndiyo hiyo tofauti yangu kwamba Mawaziri Kivuli kuchangia *immediately,* nilitaka kuona *comparison* inakuaje. Wewe utasema nini tofauti na ambacho umewasilisha? Kwa hiyo, tumeona, ahsante. Anayefuata ni Mheshimiwa Zitto, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Shibuda.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Azimio hili, kuhusiana na kupanua eneo la Hifadhi ya Gombe. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Hifadhi

ya Gombe iko ndani ya Jimbo la Kigoma Kaskazini katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kwa asilimia mia moja, na juhudi za kuongeza eneo la maji na kupunguza sehemu ya eneo la ardhi kwa ajili ya Hifadhi ya Gombe na kuimarisha uhifadhi na kuimarisha mahusiano kati ya wananchi na Hifadhi ni juhudi ambazo zilianzishwa na wananchi katika Vijiji vya Mwamgongo na Mtanga, hasa Kitongoji cha Kazinga na katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na *RCC*.

Kwa hiyo, napenda kwanza kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwamba uamuzi huu wa kuongeza eneo la maji na kupunguza sehemu ya eneo la ardhi kwenda kwa Wanavijiji ni uamuzi ambao umepitia hatua zote za wananchi. Kwa hiyo, wananchi wameshirikishwa katika hatua zote, kuanzia ngazi za Vijiji mpaka ngazi ya *RCC*. Kwa hiyo, huu ni uamuzi wa wananchi, na napenda kuishukuru Serikali kwa kukubaliana na pendekezo hili na kulileta hapa japo limechelewa, lakini angalau limeweza kufika.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008 Gombe iliingiza watalii 700 kwa mwaka. Kwa mwaka ule wa mwaka 2008 na takribani Shilingi milioni 100 tu hivi; kwa hiyo, Hifadhi ilikuwa inaendeshwa kihasara. Yaani ukiangalia mapato na matumizi ya Hifadhi, Hifadhi ilikuwa inaendeshwa kwa ruzuku kutoka

Hifadhi nyingine na hili ni tatizo ambalo tunalo takribani nchi nzima, ambapo katika Hifadhi 16 na leo tunaongeza ya 17 ya Saadan ambayo tumeshaongeza ya 17 ya Saadan katika Hifadhi zote hizi, ni Hifadhi tano tu ndizo

ambazo zinaendesha Hifadhi nyingine. Kwa hiyo, kuna kazi ya ziada ya kufanya kuhakikisha kwamba tunautangaza utalii vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Serikali na hasa Mamlaka ya *TANAPA (Tanzania National Parks)* watangaze utalii vya kutosha na hasa utalii wa Magharibi kwa maana Hifadhi ya Mahale, Gombe na Katavi na utalii wa Kusini na hasa hasa Hifadhi ya Ruaha ili kuweza kuongeza idadi ya watalii.

Lakini licha ya matatizo ambayo tunayo Kigoma ya miundombinu na kadhalika, katika kipindi cha miaka mitatu, kati ya mwaka 2008 mpaka 2011, tumeongeza idadi ya watalii kutoka watalii 700 mpaka watalii 2,600.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo ambazo tunazo, idadi ya watalii imeongezeka kutoka 700 mpaka 2,600 na kwa kweli, napenda nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhifadhi wa Gombe, Dada Noelia Myonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu anatoka Kifanya, huyu Dada Noelia Myonga, kafanya kazi nzuri sana Kigoma na ametusaidia mno, na napenda aendelee kufanya kazi nzuri Kigoma mpaka hapo tutakapoweza kuhakikisha kwamba tumeimarisha utalii pale Kigoma.

Napenda nilitaarifu Bunge lako Tukufu kutokana na namna ambavyo utalii unaongezeka Kigoma, katika kikao kilichopita cha Kamati ya Ushauri wa Mkoa, *RCC* tumeazimia kuomba Serikali Kuu itangaze uwanja wa ndege wa Kigoma kwamba, uitwe *Gombe Mahale*

International Airport kwa sababu ni uwanja wa Kimataifa unajengwa pale, kwa sababu ya kuimarisha utalii huu na juhudi ambazo zinafanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini nilikuwa naomba kitu kimoja, na nimashukuru sana Waziri Kivuli amelizungumza kwamba mwaka 1968 wakati Hifadhi hii inaanzishwa, kuna wananchi waliokuwa wanakaa pale Hifadhini na walivyoondolewa hawakulipwa fidia na ni moja ya jambo ambalo lina usumbufu mpaka leo.

Nikienda Mwamgongo au Mheshimiwa Mhonga akienda Mwamgongo kwa sababu Kijiji cha Mwamgongo ndiko ambako Mheshimiwa Mhonga ametoka, ndiko alikozaliwa na kusomea, tunaulizwa na wazee wetu kwamba kwa nini hatujalipwa fidia yetu ya mwaka 1968?

Mheshimiwa Spika, inawezekana kuwa kuna ugumu wa namna ya kufanya tathmini ya mali, mimea, nyumba na kadhalika ambazo zilikuwa pale Hifadhini, lakini Serikali ina taratibu zake za kuangalia kuweza kutoa angalau kifuta machozi kwa wazee wetu wa Mwamgongo ambao waliondoka eneo la Hifadhi kwa ajili ya kuruhusu Hifadhi kuweza kufanyika.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba, Mheshimiwa Waziri na *TANAPA,* hili waliangalie tuweze kuona utaratibu wa kufanya ili wale wazee walioondoka pale Hifadhini waweze kupata angalau kifuta machozi kiweze kuwasaidia katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mawili ya mwisho; moja ni miradi gani ambayo *TANAPA* inafanya kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi zote hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba, *TANAPA* wamejenga Shule ya Sekondari Kagongo. Nashukuru kwamba, wamejenga bweni la wanafunzi wa kike katika Shule ya Sekondari ya Bugamba. Lakini nadhani kwa sababu, utalii ni shughuli ya kiuchumi, tungeielekeza *TANAPA* ijikite zaidi kwenye shughuli ambazo zinaongeza kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Spika, sisi mwaka jana tulipeleka mradi *TANAPA.* Huu mradi ambao Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam, *Technical University of Berlin* na Serikali ya Kijiji Cha Mwamgongo, kwa ajili ya kuweka utaratibu wa *renewable energy* pale na kujenga nyumba kwa ajili ya kuhifadhi watalii. Lengo letu ni Mwamgongo pamoja na Mtanga, baadaye, lakini hatujapata ushirikiano kabisa *TANAPA* kwa sababu, wanasema kwamba, haipo kwenye *mandate* yao. *Mandate* yao, miradi yao ya ujirani mwema ni kujenga vyoo, kujenga madarasa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nadhani kuna haja ya kuimarisha nguvu kwenye *community based tourism,* ili watu wetu waweze kupata fedha. Kwamba, Mtalii akija akienda anaingia Gombe, Gombe ni Hifadhi ndogo haiwezi kulaza zaidi ya Watalii 20, lakini Watalii wanaweza wakabadilishana namna ya kuingia. Kwa hiyo, badala ya wote kwenda kulala mle ndani Gombe, wengine walale kwenye *lodges* ambazo zitakuwa Mtanga, wengine walale kwenye *lodges* ambazo zitakuwa Mwamgongo; waone pia shughuli za kiutamaduni pale.

Mheshimiwa Spika, pale Mtanga, muda mrefu sana kulikuwa kuna ngoma inaitwa Ngoma ya Mtanga, nzuri sana ya kiutamaduni ya watu wa Kigoma. Kwa hiyo, Watalii wanaweza wakaangalia pale na wakaacha fedha pale Mtanga na tukakuza uchumi, wananchi wetu wakapata huduma kama za umeme na kadhalika kama jinsi ambavyo mradi huu unaofadhiliwa na *European Union* kule Mwamgongo unavyofanya.

Mheshimiwa Spika, Mwamgongo ni Kijiji maarufu sana. Ni Kijiji ambacho kilikuwa na pesa nyingi sana. Kwa wale wananchi ambao mlikuwa mnafuatilia mpira zamani, wachezaji wote maarufu wa Kigoma, wengi walikuwa wanatoka Mwamgongo. Kama mnawakumbuka akina Wastara Baribari, kama mnawakumbuka akina Kahezi Habibu, walikuwa wanatoka Timu ya Vijana Mwamgongo kwa sababu, Mwamgongo ilikuwa inashamiri kutokana na mapato. Lakini hivi sasa kwa sababu, Ujiji imepungua na shughuli za kiutalii hazizalishi fedha, inakuwa ni vigumu sana watu wa Mwamgongo kuweza kupata fedha zakutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara na *TANAPA* tufanye *project* maalum za *income generating,* watu wetu washiriki kwenye shughuli za kitalii. Wanaoweza kusindikiza watalii wafanye hivyo, wanaoweza kufanya shughuli za kiutamaduni wafanye hivyo; wanaoweza kuuza na kutengeneza *lodges* na kadhalika kwa ajili ya watalii kulala, waweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba suala hili liweze kuangaliwa kwa umakini mkubwa sana. Naomba pia,

Mheshimiwa Waziri, huu mradi ambao tunaufanya pale na Chuo Kikuu cha Berlin na Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na Serikali ya Kijiji cha Mwamgongo, upewe kipaumbele kama mradi wa mfano. Kwa sababu, lengo letu ni kuhakikisha kwamba, tunazalisha umeme wa kutosha wa jua na kuunganisha nyumba zote za Kijiji cha Mwamgongo ifikapo mwaka 2013. Tunataka tuondokane kabisa na matumizi ya koroboi, matumizi ya mafuta ya taa. Lakini pia, tunataka tuondokane kabisa na wavuvi wote kutumia mafuta ya taa kwenye karabai, wanapokwenda kuvua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni masuala ya *renewable energy,* Wizara inaweza kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini kuhakikisha kwamba, masuala haya yanafanyika na ikawa kama ni *pilot* ya kuweza kusaidia maeneo mengine. Haiwezekani maeneo yote nchi nzima yakawa na umeme wa gridi. Kuna maeneo ambayo ni *off grid,* tunaweza tukatumia *solar,* tunaweza tukatumia *renewable*.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri kwa sababu haya maeneo ni ya kitalii, *TANAPA* inaweza ikashirikiana na Serikali za Vijiji vya Mtanga na Mwamgongo, tukaweza kuhakikisha kwamba, tumewafikishia wananchi wetu wa Vijijini umeme wa kutosha na mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Waziri, Waziri *Substantive* na Waziri Kivuli, kwa kuunga mkono hoja hii na watu wa Mwamgongo na Mtanga na Vijiji vya jirani vingine wanawashukuru sana. Naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. JOHN M. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii, ili nami niweze kuchangia katika haya machache yaliyozungumzwa ya kupitisha Maazimio yetu. Kwanza kabisa, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Kagasheki, kwa kuendeleza uaminifu na utiifu ambao ameurithi kutoka kwa wazazi wake, hususan mzee wake, Hayati Mzee wetu Balozi Suedi, ambaye ametangulia mbele ya haki na Mungu ampe pumziko la amani. Hongera sana kwa juhudi zako.

Mheshimiwa Spika, natambua Watanzania wameanza kunihoji kuhusu tetemo la afya yangu ambalo ulilizungumza jana kwamba, nilikuwa na hitilafu kidogo ya afya.

Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, pamoja na kumshukuru Katibu wa Bunge, kwa jinsi ambavyo wameweza kunihudumia wakati najaribu kurekebisha mizizi ya afya yangu isiweze kuendelea kuwa na sumu na hivyo kuwa na tetemo lingine.

Mheshimiwa Spika, naomba kushukuru sana. Jambo moja tu niwaombe na Wabunge wenzangu, tutazame uzito wetu. Nimeambiwa nipunguze kilo 26, sasa kilo 26 sio nyepesi, kwa hiyo, naomba tusaidiane, msinikaribishe kwenye mapochopocho. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kupitia hoja iliyowasilishwa hapa ya Azimio la Kupanua Hifadhi, kupitisha uamuzi wa kuongeza hifadhi, naomba kutoa ushauri ambao ni wa kuisaidia Serikali, kuibua hoja ya kutambua kwamba, Serikali, ina wajibu wa kuwa taa palipo na giza na kuhakikisha kwamba, tuna wanyamapori, pia tuna wanyama wanaoishi na binadamu yaani mifugo. Naomba sana Wizara hii

itambue kwamba, kuna maeneo mengi na sijaonana na wafugaji, Serikali, inaendelea kupanua wigo wa kuhifadhi maliasili kwa maslahi ya utalii.

Mheshimiwa Spika, lakini maeneo haya katika baadhi ya Mikoa, yamemeza maeneo yaliyokuwa na mabwawa ya maji kwa ajili, ya mifugo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, jitahidi kutafakari na kusemezana na jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi, utambue wana matatizo gani wakulima-wafugaji. Nasikitika sana kwamba, wafugaji wetu katika nchi yetu wamekuwa ni yatima wa kupata huduma kutoka Serikalini, nasikitika sana.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kweli kweli kwa sababu, haya Maazimio ya Kupanua Hifadhi hayatakwisha leo, tutaendelea kuwa tunapata Maazimio na tutaendelea kupata hii mipango, lakini nasema upanuzi wa hifadhi siukatai wala wafugaji hawakatai; lakini mwelewe, kusigana na kuzozana kati ya Wafugaji na Maafisa wanaohifadhi hii misitu yetu ya kuhifadhi wanyamapori kwa maslahi ya watalii na naomba vile vile kiu ya wafugaji itambulike.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali Kuu, itambue ina wajibu wa kuhakikisha kwamba, mifugo yetu inapata huduma sawia na zile zinazoandaliwa kufurahisha watalii. Wafugaji wetu hivi sasa ni yatima katika nchi yao kwa sababu, wanaambiwa kila siku punguzeni mifugo; mifugo hii ipunguzwe namna gani?

Mheshimiwa Spika, hakuna viwanda vya nyama. Ninaomba niikumbushe Serikali hii, wakati wa ukoloni tulikuwa na Kiwanda cha *Tanganyika Packers.* Walipokuwa

wakoloni wanawahimiza wafugaji kupunguza mifugo, walikuwa wameshawaandalia utaratibu wa masoko ya kuvuna kwa maslahi ya kuendeleza mifugo na kupunguza mifugo; leo Serikali hii, sisikii hata siku moja mnakwenda Ulaya, mkirudi hamji kusema kwamba, mmefanya mazungumzo ya kuanzishwa viwanda vya mifugo, nyama na ngozi, mnataka hawa wafugaji wafanye nini? Wawapige risasi? Waue hii mifugo? Au kuna kijicho wafugaji wasitajirike kwa kubadilisha mifugo yao kupata rasilimali pesa?

Mheshimiwa Spika, hii Serikali ya wananchi, inayojali watu, kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya Nchi na matakwa ya Katiba ya *CCM.* Ni lazima mhakikishe mnawajibika ipasavyo, ni kwa nini pana ukimya? Ni kwa nini kuna mdororo? Naomba Serikali, ihakikishe kwamba, inatutambulisha juhudi zake.

SPIKA: Ngoja kwanza nielewe vizuri. Tunazungumzia habari ya Hifadhi ya Gombe, hawa ng'ombe na nani wanaingiaje hapo?

MHE. JOHN M. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, tunazungumzia Azimio la Kupanua Hifadhi. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 63, Wajibu wa Bunge ni kuishauri Serikali. Kupitia Azimio hili, naishauri Serikali, kuhusu upanuzi wa hifadhi uendane sambamba na kutambua maslahi ya wadau wanaohitajika ambao ni sehemu mojawapo ya kutambuliwa katika masuala ya upanuzi wa hifadhi.

SPIKA: Haya, maana sijaielewa vizuri. Haya, endelea! *(Kicheko)*

MHE. JOHN M. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwamba, tunahitaji kuwa na vigezo vya kujenga mazingira ya kuhifadhi wanyamapori na hapo hapo tunahitaji kuwa na vigezo vya mazingira kwa maslahi ya wafugaji. Lakini dhulumati zinapotokea, upande mmoja utazaa kusigana na kutokana na kwamba, Serikali, imejikita upande wa utalii zaidi, lakini Wizara ya Mifugo imejisahau kutoa huduma, Wizara hizi mbili sasa wakati umefika, mkutane, mboreshe, mjenge ainisho la jinsi gani wanyamapori na mifugo itahudumiwa, ili tupende kuongeza hifadhi na kupanua wigo kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Serikali, imekuwa chungu tamu. Ukiitazama hivi sasa Serikali, leo tunashangilia sana kwamba, tumeongeza biashara ya utalii na tumeshangilia sana. Lakini kuna Maazimio ya viporo vingi yanayotokana na hizi hifadhi tunapozipanua, panatokea dhuluma kwa wanavijiji wanaozizunguka.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapoanzisha hifadhi na kupanua wigo, namshauri ndugu yangu Mheshimiwa Balozi, hebu nenda kwenye yale maeneo ukaangalie. Kauli ya mwanzo leo hapa, alipokuwa anawakilisha Msemaji wa Kamati, alitoa kauli ya kwamba, hatukupata muda wa kutosha kutafakari suala la *Saa Nane Island.* Sasa kama hawakupata muda wa kutosha, lakini baadaye wakapongeza, ni kusigana.

Mheshimiwa Spika, naomba utiifu wa masuala yetu ya kutumia wananchi tusije tena tukawa na Sheria kama ile ya

mafao ya wafanyakazi inarudi hapa Bungeni. Utoro wa imani utazalishwa na utiifu bandia wa kusema ya kwamba, tunakaa kimya kumbe tunajitia kitanzi kwa maslahi ya Watanzania ambao wanahitaji kutumia ardhi.

Mheshimiwa Spika, ardhi haizaliani. Tunapanua hifadhi, mifugo inazaliana, lakini tunahitaji maeneo makubwa kwa ajili ya biashara ya utalii. Sasa naomba kuishauri Serikali, ihakikishe wafugaji wanapata usawia wa huduma ambazo mnakazana kuzitangaza kwa ajili ya utalii. Hata wanyamapori wanaweza wakafugika kama ng'ombe. Ng'ombe tuliweza kuwachukua kutoka wanyamapori. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Balozi, ujaribu na wewe vile vile kumshauri mwenzako ni jinsi gani mtakuwa na ubora wa kutoa huduma kwa maslahi.

Mheshimiwa Spika, nimesema haya kwa sababu, naiomba Serikali, iache vioja ambavyo vipo hivi sasa. Wakuu wa Wilaya, kila siku unasikia punguzeni mifugo, mnaingia kwenye hifadhi za wanyamapori; hifadhi za wanyamapori mifugo yetu inakwenda kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mheshimiwa Waziri, *TANAPA* wana uwezo wa kushirikiana na Wizara ya Mifugo mkapunguza hizi kero, mkajenga amani na utulivu wa fikra mkaachana na fikra za kutangatanga wafugaji. Serikali ya *CCM* inapaswa kuthaminika na kusadikika, lakini vioja hivi vinaporomosha na vinazalisha machukizo. Kwa hiyo, naomba mjitambue kwamba, utekelezaji wa mambo yetu yote na hususan utekelezaji wa Serikali, hautaweza kufaulisha imani ya wananchi kuwa na utulivu kama hamtaweza kuwa na vitendo vilivyo sawa kwa mazingira ya maeneo yenu.

(Hapa Kengele ililia kuashiria kukaribia kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

Mheshimiwa Spika, hiyo ni ya mwisho au ya mwanzo?

SPIKA: Ya mwanzo. Lakini Hotuba hii sijui inaelekea wapi?

MHE. JOHN M. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, najenga uamsho wa Serikali, kujitambua. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukianza kuwa na Sera kifuniko, kwa mambo ambayo yanatanabahisha hasira za jamii, hususan wafugaji na huku tunasherehesha masuala ya hifadhi kwa kweli, tutakuwa hatuisaidii Serikali.

Nimeona nijenge kauli ambazo zitakuwa na ufunuo badala ya kuwa kifuniko kwa maslahi ya wadau wote ambao wanahitajika kuunga mkono na kuzilinda hizo hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kusisitiza usawia wa huduma. Naiomba Serikali Kuu, iache kuwa ni Serikali ya Kauli za vioja, kufuta wafugaji na hapo hapo tunashindwa kuwapa huduma, wanalazimika kuingia katika hifadhi.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipende kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, lakini pengine unipe kanafasi kidogo kumshukuru Mungu. Nichukue nafasi hii kumshukuru Mungu na pia wale wote ambao wameniletea salamu za heri na upendo kwa

kushinda kwangu kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

SPIKA: Sikujua jamani, basi Hongera. *(Kicheko)*

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Wabunge tunapoongezeka katika vyombo vya vyama tunasaidia kushauri na kujenga vyama vyetu. Niwahakikishie wana *CCM* kwamba, kwa Mkoa wa Tanga sasa umefika kwenye ngome halali na halisi, upinzani hautapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi kwa Wizara kwa kazi nzuri. Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Nitazungumza baadaye mara nyingine nitakapowapongeza ni kwa nini inaonekana hivyo.

Waendelee na juhudi hizo, walete Sera, wazijenge Sera vizuri, walete mapendekezo, watapata uhusiano na Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ningependa kuwashukuru na kuwapongeza sana *TANAPA.* Ukiona nyumba inafanikiwa, baba anafanikiwa, kuna mama nyuma yake ndiye anayemsaidia kutekeleza; Wizara imefanikiwa kwa sababu, *TANAPA* wanafanya kazi na wamefanya kazi nzuri. Tunawapongeza sana *TANAPA* kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuwapongeza wenzetu wa Upinzani, kwa mara ya kwanza nikiwa mzee katika Bunge hili, wameonesha ukomavu wa kuunga mkono pale wanapoona Serikali, inafanya kazi vizuri.

Namshukuru sana Mheshimiwa Zitto, Mchungaji Msigwa, wamezungumza vizuri sana. Wameshauri Serikali, ichukue hatua kuleta maendeleo, huo ndio upinzani; kukemea, kukejeli, hatuwezi kuijenga nchi katika msingi huo. Kwa hiyo, nawapongeza sana, moyo huo uendelee, tuendelee kushirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijawahi kufika Hifadhi ya Gombe, lakini kwa maelezo mazuri ya Waziri na wale wanaotoka katika maeneo hayo, nimekiri na nakubali kabisa mapendekezo yaliyoletwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini? Kwanza, kuna sura ya ushirikiano kati ya wananchi wa maeneo yale na maamuzi ya Serikali, kabla ya kufikia maamuzi. Kwa hiyo, hatutegemei kupata migogoro na hili ndilo linalotakiwa.

Serikali yetu ambayo inaongozwa na Chama cha Mapinduzi, hiyo ndio Sera yetu kuwa karibu na wananchi na kujenga mahusiano ambayo yanaondoa kero zao. Naipongeza sana Wizara na kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu, mimi sijafika Gombe, nitazungumza kwa ujumla tu yale mambo ambayo yametamkwa na Kamati, lakini pia yametamkwa na Waziri. Lakini mambo hayo, nitayaainisha na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati niliwahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara. Moja ya matatizo ambayo yalinipa shida sana ni ufumbuzi wa migogoro ya ardhi kati ya hifadhi na wananchi. Viko Vijiji vingi ambavyo sio tu Mkoa wa Manyara, lakini katika nchi nzima, ambavyo vinazunguka

hifadhi, hasa zile hifadhi ambazo uanzilishi wake ulikuwa wa zamani.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Hifadhi ya Tarangire, imeanzishwa kwenye miaka ya 70 kabla ya kupimwa Vijiji. Vijiji vilipopimwa na baadaye *TANAPA* kuja kupima kwa kutumia vyombo vya kisasa, pale zamani mipaka hii ilikuwa inatamkwa kwa kuangalia vilima, mito, sasa walipoleta *GPS* ikashuka chini, kufika ardhini ikaingilia maeneo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wale wamepimiwa vijiji vile, wengine wameendelea, wengine wamegoma, kwa hiyo, tunashauri *TANAPA,* kazi yao ni nzuri, kuna ushirikiano mkubwa sana kutoka *TANAPA,* mimi nimeshuhudia.

Sasa wakakae basi, walimalize hili, 2015 hatutaki migogoro, mambo madogo haya; nendeni mkakubaliane kule kwenye maeneo ambayo wananchi kwa kweli, wameishi kwa muda mrefu na bahati nzuri mmeonesha nia, basi kaonesheni kwenye maeneo yaliyobaki.

Mheshimiwa Spika, nendeni kwenye hifadhi nyingine mkubaliane, mpatane na wananchi. Pale ambapo wananchi kwa kweli wameshajikita kiuchumi, kimaisha, basi mwangalie. Rekebisheni mipaka kama tunavyorekebisha mipaka yao ya Hifadhi ya Gombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli kubwa ninalolisema ni kwamba, baada ya maelezo ya wenzangu wengi na Wapinzani, pamoja na sisi wa upande wa

utawala, kuona umuhimu wa jambo hili. Tunaunganika kabisa kuunga mkono, sasa tuwaombe wenzetu Serikalini, nendeni karekebisheni maeneo mengine ambayo yana migogoro ya ardhi kule ambako wananchi wamejikita wapewe haki, hawa ni raia wetu, ndio wanaotupigia kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitukanwa kule Manyara nikaambiwa, wewe unaona tembo ni muhimu kuliko sisi? Nikawaambia hapana na hawa tembo hawana mjomba, hawana dada, ni lazima sisi tuwatetee. Kwa kweli, wananchi walituelewa kwa kiasi fulani. Lakini lugha hii mtu mwenye kuelewa ni aliye na upeo mpana, asiye na upeo mpana atakuona wewe ni adui. Sasa twendeni tukarekebishe tujenge umoja wa nchi yetu ili chama chetu kipete.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. PAULINA P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache katika Azimio ambalo liko mbele yetu. Lakini awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Shekifu, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wetu wa Manyara, kuweza kugusia yale ambayo nilitarajia kuyazungumzia mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna usemi wa Kiswahili unasema kwamba, Ukiona Jumbe anapita, hapo hapo ueleze kinachokusibu. Baada ya kuona Azimio hili, nikaona ni wakati pekee wa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, kuhusu matatizo ya Hifadhi ya Tarangire, ambayo Mheshimiwa Shekifu, ameweza kuyagusia.

Mheshimiwa Spika, ni jambo zuri sana...

SPIKA: Mheshimiwa Gekul, kwa mujibu wa taratibu zetu, hata kama Mheshimiwa Shibuda alikwenda nje kabisa, naomba tujadili hoja yenyewe. Tukianza tena manini yote, basi tutaingia kwenye matatizo kabisa; tujadili hii ya Gombe kwanza.

MHE. PAULINA P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nina-*relate* haya ninayozungumza na mjadala ambao uko mbele yetu. Ninachopenda kusisitiza ni kwamba, katika mjadala huu wa kuongeza mipaka hii ya hifadhi, kuna mambo ya kujikumbusha; maana hili limefanyika katika hifadhi hii ya Gombe, lakini busara hii ndicho ambacho napenda kuzungumzia.

Mheshimiwa Spika, kwamba, wakati Mheshimiwa Waziri, anazungunza haya kwamba, kuna maeneo ya mashamba yalikuwepo katika hifadhi hii, kuna maeneo ya makaburi, lakini kuna nyumba saba zilikuwepo, busara ikatumika. Wakaona kwamba, haya maeneo wayaweke pembeni, ili wasiingie kwenye migogoro na wananchi, migogoro ambayo sio ya lazima.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, hili zoezi ni endelevu la kuongeza mipaka hii. Lakini nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba, wameanza vizuri, wametumia busara kuweza kuona kwamba, inapobidi pale kusiwe na sababu yoyote ya kusumbua wananchi, basi busara zitumike. Kwa hapa busara imetumika, lakini nimkumbushe

kwamba, kuna maeneo mengine ambayo hizi busara zinahitajika na nimetoa mfano wa Hifadhi ya Tarangire.

Mheshimiwa Spika, si vibaya kutoa mifano wakati unajadili jambo husika. Naomba nikumbushe tu kupitia mjadala huu kwamba, hizi busara ambazo mmezitumia Kigoma, ni lini zitakuja kutumika Manyara?

Mheshimiwa Spika, mara nyingi nimekuwa nikilikumbusha hili kwa sababu, matatizo ya wananchi yanapokuwa yanadumu kwa muda mrefu Serikali, haichukui hatua wananchi wanakata tamaa, wanaona kwamba, hakuna msaada wowote ule. Nalisema hili, Mheshimiwa Shekifu amezungumza kwamba, kuna baadhi ya Vijiji, naomba niendelee kuvitaja kwa sababu, naendelea kuvitaja mara kwa mara Gijedabu, Ayamangu, Gedamar, Kaya zaidi ya 240 hawana makazi, hawaruhusiwi kuendeleza maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kama hili limefanyika Gombe. Kama hili limewezekana, niombe tu Wizara kwamba, sasa baada ya kulimaliza hili muweze kuwatembelea wale wananchi wapate eneo mbadala, waweze kutulia kwa sababu, hawaruhusiwi kuendeleza maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kutoa mfano huo, niende kwenye kipengele namba mbili (2), kipengele ambacho napenda kukizungumzia, suala la zile Kanuni; hifadhi imepanuliwa, maeneo yameongezeka ya hifadhi, lakini niikumbushe Wizara kwamba, kuna Kanuni ambayo katika Bunge lililopita, Bunge la Nane, nilizungumza Kanuni ambazo zinatumika sasa kuweza kulipa fidia kwa yale

maeneo ambayo yanapakana na hifadhi hizo. Zile Kanuni, zinatakiwa zirejewe upya na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri, wakati anajumuisha katika Bunge la Bajeti, alisema kwamba, hizo Kanuni zingeweza kutazamwa upya.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe rai yangu na niendelee kuikumbusha Wizara kwamba, zile Kanuni bado ni gandamizi kwa wananchi. Kwa sababu, unapokuwa unapakana na hifadhi, kama Kanuni zinasema kwamba, mita 500 kutoka pale unalipwa sifuri kama mashamba yako yamevamiwa na wanyama, bado wale wanakijiji wanakuwa wamewekwa pale kwa mujibu wa Sheria za Vijiji. Lakini wanakuwa hawapati hizo fidia kwa sababu ya hizo Kanuni, ambazo hazijaangalia kwa makini kwamba, wale wananchi walikuwa wamewekwa pale kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili nalisema kwa sababu, hifadhi hii ya Gombe, leo inapanuliwa, inaongeza wigo.

Lakini pia, niikumbushe tu Wizara, kwamba, baada ya Azimio hili, basi mtuletee mapema hizo Kanuni tuzione kwa sababu, naamini miongoni mwa maeneo ambayo yanapakana na hifadhi na kuna wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kama wasemaji wengine walivyotangulia, wale wafugaji mifugo yao inapokuwa imeathiriwa na wale wanyamapori ambao tunawahifadhi, fidia wanazopata, mfano mbuzi 25,000/=, leo huwezi kupata mbuzi wa kiasi hicho, lakini ng'ombe 50,000/= kwenye Kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, vitu kama hivyo vinakuwa vinawakwaza wananchi kwa sababu, ng'ombe huyo huyo ukienda kwenye mnada au popote ni zaidi ya 300,000/=. Lakini kwa sababu tu, ameathiriwa na wanyamapori ambao wako katika hifadhi hizi, Kanuni zinawabana alipwe kiasi hicho labda 50,000/= ni kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie hili suala la Kanuni kwa upana wake kwamba, baada ya Azimio hili, Mheshimiwa Waziri, muone ni jinsi gani mnarekebisha hizo Kanuni mapema sana kwa kuangalia hali halisi ambayo inawasibu wakulima hawa na wafugaji hawa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimkumbushe au nikumbushe ombi hili ambalo tulililitoa kwa Waziri wa Nishati na Madini tarehe 17 Septemba, wakati ametembelea Babati pale, tulipozungumzia matatizo ya Hifadhi ya Tarangire na jinsi ambavyo vijana wanaochimba madini wanapata matatizo hayo. Vijana wale wa vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Tarangire, wanalipa 1,500/= kila siku anapokwenda kuchimba madini.

Pamoja na kwamba, ana leseni lakini kwa sababu anakatisha katikati ya hifadhi, inabidi kila siku anapokwenda kufanya kazi zake alipe 1,500/=. Mheshimiwa Waziri, aliahidi kwamba, angeongea na Waziri wa Maliasili.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia siku hii ya leo nikumbushe kwamba, bado tunahitaji tuone kwamba, hilo linarekebishwa. Hili halitofautiani sana na mahusiano ya hifadhi, kwamba, kunakuwa na wananchi ambao shughuli zao inawezekana za uvuvi au za madini au shughuli nyingine, wanakuwa wanakatisha katika maeneo ya

hifadhi; Mheshimiwa Waziri, ni vizuri sana hayo mahusiano yakaangaliwa kwa karibu, ili upande mmoja au mwingine usiathirike na zoezi zima la kuhifadhi maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nishukuru sana na niseme ni jambo zuri sana. Lakini hii busara ambayo imetumika sasa katika hifadhi hii ya Gombe, basi tuombe sana kwa yale maeneo yenye migogoro Mheshimiwa Waziri, mjitahidi kupitia yale maeneo na muone ni jinsi gani ambavyo mnaweza mkamaliza matatizo hayo kupitia busara hii. ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya kuunga mkono Azimio la Upanuzi wa Hifadhi ya Gombe. Kwanza, niipongeze Wizara na kwa kweli tumechelewa maana tulihitaji jambo hili muda mrefu uliopita.

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa Gombe, watakaofaidi zaidi ni wananchi wa Mwamgongo na Mtanga. Ukiangalia bado maeneo yao hayajachukuliwa; angalia eneo la Kaskazini kwenye ramani pale, kwenye eneo la Kusini, hata yale maeneo ambayo yalikuwa ni ya muhimu kwa maana ya maeneo ya zile nyumba saba, unaona kuna makaburi na eneo ambalo watafanya shughuli zao limeondolewa nje ya sehemu ya hifadhi. Nampongeza sana Waziri kwa kuja na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, la pili, niishukuru Wizara kwa maamuzi makubwa haya ya kupanua Hifadhi ya Gombe, maana moja kubwa katika mambo makubwa ambayo yamefanyika watalinda mazalia ya mazao ya samaki na dagaa na maana yake ni moja tunalinda mazalia haya kwa ajili ya vizazi vijavyo, tukiendelea na hivi tunavyokwenda iko hatari vizazi vinavvyokuja wangepata matatizo sana katika kupata samaki na dagaa na hali imeanza kuonekana. Kwa hiyo, niishukuru sana Serikali kwa kuamua jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lingine ni pamoja na mambo mazuri Serikali imeyafanya, sisi pale *RCC*, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Rais alipokuja Kigoma katika mambo ambayo tulimwomba na nadhani alikubali, ni kujenga barabara sasa ya Mwandiga, Kagongo, Kakele, Mwamgongo mpaka Kagunga ambayo ni kilomita 28. Hadi sasa wenzetu wa *TANAPA* washiriki katika kazi hii njema, kama vile ambavyo *TANAPA* wanajenga barabara zinazopita mbugani kwa maana ya Serengeti, na maeneo mengine yote.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni moja tu, tukijenga barabara hii siyo lazima maana wako watalii wasingependa kupanda boti tunawapa *option* nao ya kwenda kwa njia ya barabara. Kwa sababu hiyo hata lile zoezi letu la kuendeleza bioanuwai ya Ziwa Tanganyika itakwenda kwa kasi kubwa zaidi. Kwa hiyo, niwashukuru sana na niwaombe Wizara washiriki kwenye kazi hii ya kuhakikisha barabara hii tunaipata muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Spika, pia nimwombe Waziri, mmefanya maamuzi makubwa ya kupanua Hifadhi ya Gombe, niwaombe sasa mkisoma Azimio lenu unaona nia njema, unaona jambo ni jema na limefikiriwa vizuri, lakini sasa tuombe sana upanuzi wa Gombe uendane na watalii kuja wengi Kigoma na ili wananchi wa pale waone kwamba, unaona tulikuwa tunapata watalii 20 labda kwa siku, baada ya kupanua Hifadhi hii, sasa tuna watalii 100, tuna watalii 200. Maana yake ni moja tu, fedha itaongezeka kwenye uchumi wa watu wa Kigoma, ajira itaongezeka kwenye uchumi wa watu wa Kigoma, kwa hiyo, maana hiyo jambo hili litatusaidia kama nchi.

Mheshimiwa Spika, maana ukiangalia *statistics* za *tourism* Rwanda, wana sokwe mtu, wanaingiza fedha nyingi sana, sisi tuna sokwe mtu wengi zaidi kuliko hicho kinchi kidogo. Kwa hiyo, maana yake ni nini, ni kwa sababu ya sababu zilizokuwepo huko nyuma, lakini kwa sababu mmeamua kuzisahihisha sasa, ni vizuri tuhakikishe sokwe mtu hawa walioko Kigoma wanatangazwa vya kutosha ili waweze kuleta watalii wengi zaidi Kigoma.

Mheshimiwa Spika, pia niwaombe *TANAPA* waendeleze mashirikiano na wananchi wa vijiji vile, mashirikiano yasiwe wakati huu tu wa kupanua hifadhi. Baada ya kupanua Hifadhi tukaanza kusikia migogoro kila kukicha, nyie mnajua lazima kama hatujajenga ile barabara sehemu ya kupita ni hiyo hiyo hapo ukiwa unakwenda Mwamgongo mpaka Gunga mpaka Burundi na kuna watu wengine watakuwa wanapita hapo wanakwenda sehemu ambazo wanakwenda kufanya

shughuli zao za uchumi. Kwa hiyo, ningeomba mashirikiano yaongezeke zaidi ili jambo hili jema liwe na maana kwa wananchi wa Wilaya ile.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni ulinzi katika maeneo ya Ziwa Tanganyika, tumekuwa na matatizo makubwa sana katika Mkoa wa Kigoma kwa uvamizi wa kijambazi katika maeneo ya Ziwa Tanganyika. Mheshimiwa Waziri hili naona unalifahamu, ulivyokuwa Wizara ya Mambo ya Ndani kama jambo tulikuwa tukikuuliza kila siku, ni suala la ulinzi katika Ziwa Tanganyika, ningeomba sana, sasa tumepanua maeneo haya, basi watu wajue eneo hili lina mwenyewe, wasiwe wanakuja tu wananyang'anya vifaa vya watu vya kwenda kuvulia samaki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimshukuru sana Waziri kwa kuleta Azimio hili na niwashukuru Wabunge wenzangu ambao tumeliunga Azimio hili, ni jambo jema na kweli hii ndiyo kazi ya Chama cha Mapinduzi. Nashukuru sana na naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala, lakini mzingatie Azimio siyo kwenda nje kwenye mifugo.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi nakuahidi nitazingatia Azimio.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Azimio hili, ni jambo jema kama wanavyosema wenzangu, lakini pia naomba nitoe angalizo kwamba, kwa sisi Wabunge ambao tunakaa hapa leo kwa lengo la kupitisha Azimio hili ni lazima tuwe macho

na tuwakumbushe wenzetu katika Serikali kwamba tunapozidi kupanua mipaka kama alivyokuwa akichangia mwenzangu Mheshimiwa Shibuda hapa na hata mchangiaji mwingine Pauline Gekul, kwamba, tunapoendelea kutanua mipaka yetu ya hifadhi maana yake ni kwamba tunazidi kuwa-*dominate* wananchi, tunazidi kuchukua maeneo ambayo pengine kuna wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa natoa angalizo tu kwamba, yasije yakatokea yale ya lile Azimio la *NSSF* baadaye wananchi wakaanza kulalamika, nitoe ushauri kwa Serikali kwamba wajipange vizuri kuhakikisha wanapokwenda kutanua mipaka ya hifadhi, basi maslahi ya wananchi yawe yamezingatiwa ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima sana. Nalisema hili nikizingatia katika Jimbo langu kule maeneo ya Ishiki, Kimiziwa, Ugembe two, Ipala kuna migogoro mikubwa sana ya ardhi ambayo imesababishwa na utanuzi wa hifadhi.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake imekuwa ni ku-*dominate,* wananchi wanaishi katika vijiji vile ambavyo vimesajiliwa miaka ya 60 na 70 na wameishi pale maisha yao yote, wamezaa watoto na wamepata wajukuu katika maeneo yale.

Leo hii inatokea kwa ghafla, wanaambiwa mipaka ya Hifadhi imeongezeka, kwa hiyo, wananchi wanatakiwa waondoke katika maeneo haya ambayo wamekuwa wakishi kwa miaka yote.

Mheshimiwa Spika, hili kwa namna yoyote ile halikubaliki na mimi kama kada wa Chama cha Mapinduzi

naliona ni jambo linaloweza kutia matata kidogo mwaka 2015 kwa wapiga kura ambao ni *loyalist* wakubwa sana wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tu nitoe angalizo hilo. Nikumbushie tu takriban miaka 15 iliyopita, nikiwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Kigoma, nilifika Gombe Mahale kupitia taasisi ya Dkt. Jane Guido ambaye alianzisha *NGOs* na mimi nilikuwa mwanachama. Nilikuta ni mahali pazuri, pana uoto mzuri wa asili, kuna sokwe mtu wakubwa sana ambao huwezi kuwaona katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nawahamasisha Waheshimiwa Wabunge wafanye *tourism* ya ndani, waende wakatembee Gombe Mahale, waweze kujionea hifadhi maliasili ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Azimio hili la kuboresha na kuhuisha mipaka yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Kwa matumizi mazuri ya muda, naona sasa nasitisha mjadala huu na namwita mtoa hoja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa mjadala ambao umejitokeza baada mimi kutoa hoja ambayo nimeitoa kuhusu Hifadhi ya Gombe.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hapa kwa maneno ambao ni Mheshimiwa Lembeli, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Shibuda, Mheshimiwa Shekifu, Mheshimiwa Gekul, Mheshimiwa Serukamba na Mheshimiwa Dkt. Kigwangala.

Mheshimiwa Spika, pia niwahakikishie wale Waheshimiwa Wabunge ambao wametoa michango yao kwa maandishi kwamba, tutafanya kila jitihada wapate majibu yao na hatukuweza kuwa na muda wa kutosha kuweza kuyatafakari haya.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, nazingatia vizuri sana michango ya Waheshimiwa Wabunge na naiheshimu kabisa, lakini Waheshimiwa Wabunge Azimio tunalolizungumzia hapa ambalo nimeliweka mezani mlitazame, mlijadili, linapunguza mipaka na linaongeza mipaka, linapunguza mipaka kwa kutazama maslahi ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimeongeza mipaka bila kuathiri Mtanzania yeyote, hatukukugusa Kijiji wala hatukugusa ardhi. Sasa nazingatia ukweli kwamba, yapo hayo ambayo yamekuwepo na wala siyo ya leo, lakini Waheshimiwa Wabunge, niombe mtufuatilie kwa ukaribu zaidi na mtambue hata yale mazuri tunayoyafanya.

Najua kabisa niliwaambia kwamba, masuala ya migogoro ya ardhi baina ya Hifadhi na wananchi tunayapa uzito mkubwa sana na nikawaambia kwamba, nimeweka Kamati Maalum ambayo inapita pote na imo katika

utaratibu huo. Hili nataka niwahakikishie wale ambao nawasikia mnazungumzia 2015, mimi huko siko. *(Makofi)*

Suala hapa tunazungumzia haki za Mtanzania, hatumpi haki Mtanzania kwa sababu ya 2015, tutampa haki na ndiyo maana nasema tusiwe na hofu, kikubwa muwe na imani na Serikali, tumefanya na tutazidi kufanya. Tumekwenda tumeunda Tume na inapita na ndiyo kwa mfano, kama hili suala la Gombe tumeona kabisa kuna masuala ya makaburi hapo. Kuna masuala ya nyumba za watu na kadhalika. Kwa hiyo, maeneo yale tumeona hapana, tuwaachie wananchi kwa sababu ni kitu ambacho kinaleta kero na hilo tutakwenda nalo mahali pengine.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu nimesikiliza michango ya Wabunge ambao kwa kweli nasema, tuna haki ya kutoa michango ambayo tunataka kuitoa Bungeni, lakini inatia wasiwasi, tunapotoa michango ambayo inaweza ikaleta vurugu kidogo kwa watu unapoanza sasa kuzungumza kwamba Serikali haijali, haijali wafugaji, ukasema kwamba Serikali inajali watalii peke yake, nadhani hamtutendei haki, nadhani kwa nini tusijali wananchi wetu, Serikali gani hiyo isiyojali wananchi wake jamani? Haiwezekani na ndiyo maana tunasema kwamba, haki itatendeka na haya masuala yanatazamwa kwa upana wake na jitihada kwa kweli zinaonekana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, lakini pia niwatoe wasiwasi wananchi wa Tanzania ambao wanatusikiliza, siyo kwamba

Serikali itafanya mambo kwa sababu ya kutegemea kitu fulani hapana, tutafanya kazi kwa sababu tunajua ni haki yao. Kwa sababu hiyo, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko, tumetengeneza Tume na Tume hiyo imeshaanza kazi, inazunguka, imeshakwenda mahali pengi, itatuletea hiyo na tutaweka utaratibu wa kutazama haya maeneo na kwa namna gani?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunazingatia hizi hifadhi zilipowekwa idadi ya Watanzania ilikuwa kiasi fulani, sasa hivi tunatazama ile *pressure* inayokuwepo kutokana na ukuaji wa *population* ya watu na mifugo na kadhalika. Mimi naomba tu haya mambo tuyajadili vizuri kuliko kujaribu sasa kuamsha hisia za watu na kuwajengea watu hisia za kuonekana kwamba, Serikali haina mambo ambayo inafanya, ambapo siyo kweli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mwaka 1968 la eneo la Gombe na wananchi ambao walikuwa wameahidiwa kwamba, wangepewa fidia na mpaka leo hawajapata fidia, niseme kwamba, hilo suala nimelichukua. Kwa kuwa labda hapa katikati nadhani lilikuwa halijakumbushwa ama halijasemewa, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Kabwe Zitto na nimhakikishie Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, kwamba, hilo jambo tumelichukua, tutalitazama katika historia yake, tutatazama kulikuwa kuna nini ili tuone wananchi hao wanatendewa haki yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi ambao ameuzungumza Mheshimiwa Kabwe Zitto ambao ni mradi ambao anasema kwamba wamejaribu kushirikisha *TANAPA*

lakini *TANAPA* wamekuwa wagumu. Niseme ndiyo tunausikia huu, lakini kwa kweli mantiki ya kushirikisha wananchi ambao wanazunguka hifadhi ni muhimu sana. Kama hizi hifadhi zitakuwepo na zitaendelea kuwepo maana yake walinzi wakubwa wa hizi hifadhi zetu na walinzi wakubwa wa wanyamapori wetu ni wale watu ambao wanazunguka hizi hifadhi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunasema kuwe na ujirani mwema ama tuwe na ushirikishwaji mkubwa kuhakikisha kwamba na sote ni Watanzania na hizi rasilimali zote na maliasili ni za Watanzania wote na wala siyo kwamba ni za kundi fulani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwahikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, hilo kwa kweli tutalifanyia kazi kwa sababu unapowashirikisha na mkawa na vitu ambavyo vinazalishwa, vinajenga ajira kwa watu, vinajenga uzalishaji na kadhalika, vinamtoa pia Mtanzania katika umaskini. Kwa hiyo, niseme kwamba, hiyo kwa kweli tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la kutangaza utalii, kwa kweli, hilo tumelipokea na tutaendelea kulifanyia kazi na tumekuwa tunazungumza huko nyuma, nadhani mazungumzo hayasaidii sana isipokuwa tutaendelea kufanya kwa vitendo ili tuone kwamba, tunakwenda mbele kwa idadi lakini pia na kwa ile *quality* ya *tourism* ambayo tutaweza kuitoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani,

nataka pia nimhakikishie kama Waziri wa Maliasili na Utalii amesema kwamba labda kuna mambo ni *personal absolutely,* siamini kabisa kwamba *there is anything person, we did know each other before coming to this Parliament,* kwa hiyo, sidhani kama kuna kitu chochote na kwa kweli unapozungumza *we respect* na *concern* yetu kubwa na nafikiri itakuwa ni ya kwako, ni kwamba, yale ambayo tunayazungumza yawe kwa kweli ni ya kujenga na pia yasiwe mambo ambayo yanaweza yaka-*insight* na kuleta *some kind disorder* katika *society* au katika *community*. Lakini kwa mfano, mambo haya ambayo umezungumzia kuhusu meno ya tembo, wamekamatwa huko Hong Kong lakini pia umezungumzia meno ambayo yamekamatwa hizi siku mbili, siku tatu na hii ikaonyesha kwamba ni karibuni.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Msigwa na niliambie Bunge lako Tukufu, lakini pia niwaambie Watanzania, hii *consignment* ambayo imekamatwa kule na mpaka sasa hivi bado hatujawa na uhakika tumo katika mazungumzo, Balozi wetu Beijing, China yupo na hata jana nimezungumza naye, pia juzi nimezungumza naye. Lakini pia *IGP* wetu na *Police system* wako na Waziri wa Mambo ya Ndani yupo hapa na ni suala ambalo tumelizungumzia jana, tumelizungumzia juzi na siku za nyuma.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kinatuletea tatizo hapa ni kwamba, ripoti za kule Hong Kong zina utata kwa maana ya kusema kwamba, haya meno *origin* yake ni wapi? Kwa sababu ziko kontena mbili;

Wao wanasema kontena moja inaelekea kwamba ilitokea *Democratic Republic of Congo* na kontena ya pili

inaelekea ilitokea Tanzania, lakini wapo ambao wanasema hata hiyo kontena ya pili inaonekana Tanzania ilikuwa ni *transit*.

Sasa kitu ambacho sisi tunajaribu kukifuata Mheshimiwa Msigwa ni utaratibu tu, tunataka kujua kama zile kontena zili-*originate* kutokea Tanzania, lakini pia tunataka kujua kama meno yale kutokana na *DNA* ambayo wanajaribu kufanya, ni ya Tanzania, lakini tulikuwa tunataka kujua pale *custom* kwetu, ni watu gani walikuwa zamu wakati ule, ni watu gani maana yake hivi vitu viko *documented* tunataka kujua nani waliruhusu au nani walifanyaje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, taratibu ambazo tunazifanya wala siyo kwamba tunazembea katika jambo lolote, lakini yote haya yanatokea ni kukuonesha kwamba sasa hivi ndani ya Wizara tunafanya kazi na ndiyo maana yanajitokeza na tutawaondolea. Lakini pia tutakaribisha ushauri mzuri, mawazo mazuri ya kutusaidia kuboresha kwa sababu hizi ni mali za Watanzania ambao sote kwa kweli tuna joto la kusema kwamba, hapana lazima uhifadhi uwepo. Hili nakubaliana na wewe kabisa, tusishughulikie upande wa kukamata, lakini tushughulikie upande wa kuzuia. Kwa hiyo, hilo nakubaliana nalo na kweli hilo tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hoja ambazo zimetolewa, naona nyingi, kusema kweli utanisamehe na naisema hii kwa heshima kubwa sana na kwa unyenyekevu mkubwa sana, hapa si mahali pake.

Niseme tu kwamba nimezichukua bado tutazifanyia kazi na kwa kweli tunazifanyia kazi, lakini sidhani kwa mfano za kuchimba madini ndani ya hifadhi, hilo ni suala kubwa zaidi kuliko Mheshimiwa Gekul alivyolitamka, bado tunalifanyia uchunguzi wa aina yake.

Mheshimiwa Spika, kuna watu nataka hata hapa niseme kabisa *as we go along,* kuna watu ambao tunajua kabisa *even* ndani ya *TANAPA* wamo, hili ni suala kubwa zaidi, kwa hiyo wewe umezungumzia suala dogo la watu wapate vibali vya kupita na kutoka, lakini sisi tunazungumzia suala kubwa zaidi la kusema kwamba, kinachofanyika kule si sahihi kwa mujibu wa sheria tulizonazo na kadhalika. Lakini tunayoyafanya ni katika jitihada ya kuona kwamba mambo yanakwenda sawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mheshimiwa Serukamba na kuhusisha *TANAPA,* hilo kwa kweli tumelipokea tutazima jinsi tutakavyoweza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, niseme kwa ujumla hoja nyingi ambazo Waheshimiwa Wabunge mmezitoa, kwa kweli nataka niwahakikishie na wananchi wanaotusikiliza katika hoja ya Gombe, hakuna eneo ambalo tumelichukua, tulilochukua ni eneo la maji na ukitazama faida zake ni kubwa zaidi kuliko hasara ambazo watu wanaweza wakazifiria.

Mheshimiwa Spika, huku katika maeneo mengine tumeyaacha kwa wananchi na kama tulivyosema tumeona kwamba, ni busara na katika maeneo mengine tutafanya kwa kutazama na ile Tume ambayo inakwenda ili tuone tutafikia maamuzi gani.

Lakini kubwa nataka wananchi wajue kwamba, Serikali hii ipo kwa maslahi yao, ipo kwa faida yao, ipo kwa kusimamia haki zao na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, kwanza niseme kwamba, nashukuru sana na niombe kwa mara nyingine ya pili naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Marekebisho ya Mpaka na Upanuzi wa Hifadhi ya Gombe liliridhiwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kama alivyosema Mheshimiwa Waziri nadhani Maazimio ya leo yalikuwa yanaeleweka sana kwa hiyo, nikaona kwamba sasa watu wanakwenda tu kujisemea na vitu vingine ambavyo havihusiki. Kwa hiyo, tutumie vizuri muda wetu huu. Shughuli za leo zimekwisha, kwa hiyo, naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 6.50 Mchana Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 1 Novemba, 2012 Saa Tatu Asubuhi)